**AUA** mke naye ajiua, mwingine akamatwa tuhuma za mauaji

UKURASA 3



**MWAIPAYA** apewa mbinu kufanikisha utendaji kazi u-DC

UKURASA 4


RAIS SAMIA ALIVYONG'ARISHA DIPLOMASIA, UJIRANI MWEMA

siasa

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

Rais Samia na bajeti inayowajali wanawake

SIKU 100 IKULU...

'DAKTARI' SAMIA ALIVYOUTIBU UTAPIAMLO WA SIASA, UCHUMI

UKURASA 11


# Nipashe

Jumatano Juni 30, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580627

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710


# ADHABU KALI

**KWA** wanaosababisha kelele za sauti na mitetemo makazi ya watu, walengwa wakuu watajwa...*Endelea Ukurasa wa 2*



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, wakati akitoa taarifa kwa umma ya udhibiti wa uchafuzi wa mazingira utokanao na kelele na mitetemo. Kulia kwake ni Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima. Wengine (kutoka kulia) ni Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Pauline Gekul, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Khamis Chilo, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Wenye Ulemavu), Ummy Nderiananga na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga. **PICHA: OMR**

## Kifungo cha Zuma jela chaibua mjadala mzito

UKURASA 19

UKURASA WA 2

### MHANDISHI MFUGALE AFARIKI DUNIA



MTENDAJI Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mhandisi Patrick Mfugale...

## WATUMISHI 102,630 WAPANDA MADARAJA

UKURASA 2



Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa (kulia), akimkabidhi Rais mstaafu wa awamu ya nne Dk. Jakaya Kikwete Mpango Mkakati wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa miaka mitano 2021/22-2025/26, baada ya kuzindua jijini Dodoma jana, unatarajiwa kutumia Sh. trilioni 114.8. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

**MICHEZO** **KARIA AUPIGA MWINGI UCHAGUZI WA URAIS TFF** UK. 24

**MAONI, KATUNI UK. 6**

HABARI KITAIFA

# Kibano kelele nyumba za ibada, starehe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetangaza kutoa adhabu kali ikiwamo kifungo cha miezi sita jela na kufungiwa biashara kwa watu watakaobainika kusababisha kelele na mitetemo kwenye makazi ya watu hasa kwenye nyumba za ibada na starehe.

Hatua hiyo ni moja ya mikakati iliyofikiwa na mawaziri wanane katika udhibiti wa kelele na mitetemo ambayo imekuwa ikiwabughudhi wananchi katika maeneo ya makazi.

Mawaziri hao ni kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Akitoa tamko hilo kwa waandishi wa habari jana jijini hapa, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, alisema hatua hiyo imetokana na hivi karibuni kuwapo ongezeko kubwa la kero hizo nchini.

Jafo alisema wizara hizo zimekuja na mikakati mitano yenye lengo la kuondokana na hali hiyo.

Alitaja mikakati mingine kuwa ni pamoja kutilia mkazo utekelezaji Kanuni za Usimamizi wa Mazingira za mwaka 2015 zinazotoa adhabu ya faini ya Sh. milioni moja au kifungo kisichozidi miezi sita.

Waziri Jafo alisema Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea kuzifanyia kazi kanuni za adhabu za makosa ya uchafuzi wa mazingira ili kuongeza ukali wa adhabu za uchafuzi wa mazingira nchini.

"Kila mwananchi ahakikishe shughuli wanazofanya hazisababishi kero ya kelele na mitetemo, wamiliki wa nyumba za ibada na kumbi za starehe na burudani wahakikishe sauti zitokanazo na shughuli zao hazizidi viwango vinavyokubalika kwa mujibu wa sheria," alisema.

Pia alisema wamiliki wa maeneo ya burudani na starehe wazingatie matumizi ya vipimo vya kelele na vizuia kama ilivyoelekezwa kwenye masharti yote ya leseni zao.

Kuhusu ongezeko la utoaji wa taarifa za malalamiko, Jafo alisema kwa mwaka 2019/20 NEMC ilipokea malalamiko 165 kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Mbeya, Mwanza, Morogoro na Tabora ambayo yalihusisha kelele kutoka kwenye nyumba za ibada, kumbi za starehe na baa.

"Katika kipindi cha Januari mpaka Machi 2021, NEMC walipokea malalamiko 93 kutoka kanda mbalimbali, kanda ya kati (30), kanda ya kaskazini (12), Kanda ya Ziwa(21), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini(6), Kanda ya Mashariki(31)," alisema.

Alisema katika kipindi cha Januari hadi Aprili 2021, jumla ya malalamiko 20 yaliripotiwa katika Jiji la Dodoma na kuzitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia utekelezaji wa kanuni hizo.

Naye Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alisema takwimu za shirika linalosimamia mazingira katika bara la Ulaya zinaonyesha kuwa kelele husababisha vifo vya mapema vya watu 16,600 na wengine 72,000 hulazwa hospitalini kila mwaka kutokana na madhara ya kelele.

"Napenda kuelimisha wananchi kuwa kelele zilizopita kiwango stahiki cha afya ni chanzo cha magonjwa ya hatari, ikiwamo kupungua kwa uwezo wa ubongo kufikiri na kuchanganua mambo kwa wakati, kushindwa kupata usingizi wa kutosha unaostahili kwa afya ya mtu husika hivyo kusababisha msongo katika afya ya akili na mifumo ya afya kwa ujumla," alisema.

Aidha, alisema husababisha magonjwa mbalimbali yakiwamo ya moyo, shinikizo la damu, maumivu ya kichwa, uharibifu wa muda au wa kudumu wa masikio.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan, akifungua Kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama hicho (NEC), jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Watumishi 102,630 wapandishwa madaraja

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WATUMISHI wa umma 102,630 wamepandishwa madaraja huku serikali ikionya kuwachukulia hatua maofisa utumishi ambao hawakuwasilisha majina ya watumishi kwa ajili ya kazi hiyo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, alisema maofisa hao watachukuliwa hatua kwa kushindwa kutekeleza agizo hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Waziri Mchengerwa alisema idadi hiyo imezidi ile ilivyokuwa kwenye bajeti ya awali ambayo serikali ilipanga kupandisha madaraja watumishi 91,000.

Mchengerwa alisema watumishi wote wanaostahili kupandishwa vyeo wanatakiwa wapandishwe kwa sababuni haki yao kulingana na vigezo walivyo navyo.

"Sitasita kuchukua hatua kali maofisa utumishi watakaozembea na waliozembea kuwasilisha majina ya watumishi ambao wanastahili kupandishwa lakini hawakufanya hivyo," alisema.

Alitoa rai kwa watumishi wote wanaostahili kupandishwa vyeo wapandishwe na ikigundulika kuna ofisa utumishi aliyefanya uzembe nakusababisha mtumishi aliyestahili hajapandishwa, atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Kuhusu uzinduzi wa mtandaokwa ajili ya watumishi wa umma kuwasilisha malalamiko yao, alisema mfumo huo utajulikana kwa jina la 'Sema na Waziri wa Utumishi' na utamsaidia mtumishi kuwasilisha maoni yake bila ya kusafiri kufika eneo husika.

Mchengerwa alisema mtandao huo utasaidia kuondoa mzigo wa watumishi waliokuwa wakisafiri kutoka mikoani kwenda wizarani kupelekamalalamiko yao. Alisema hivi sasa mtandao huo utawasaidia kutoa kero zao wakiwa mahali pao pa kazi.

"Hivi sasa malalamiko, mapendekezo na maoni ya masuala yote yanayohusu wizara yetu yanashughulikiwa kwa njia ya mtandao. Si lazima mtu asafiri kuja hapa. Akituma malalamiko yake yanapokewana kushughulikiwa ikiwamo kupewa majibu papo papo," alisema Mchengerwa.

Alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan kwamba anataka mpaka anamaliza muda wake wa uongozi, aone malalamiko ya watumishi wa umma yawe yamekwisha.

## Mhandisi Mfugale afariki dunia

**Na Romana Mallya**

MTENDAJI Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mhandisi Patrick Mfugale, amefariki dunia jana asubuhi jijini Dodoma.

Msemaji Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Idara ya Habari (Maelezo), Gerson Msigwa alithibitisha jana kuwa kifo hicho kilitokea asubuhi.

Enzi za uhai wake, Mhandisi Mfugale ametumia muda wake mwingi kama mtaalamu wa madaraja.

Alibuni daraja la Magarasi lenye urefu wa mita 178 kwa Sh. milioni 300 na baadhi ya madaraja aliyojenga ni pamoja na daraja la Mkapa Rufiji, daraja la Umoja linalounganisha Tanzania na Msumbiji huko Mtwara.

Mengine ni daraja la Rusumo huko Kagera, daraja la Kikwete lililoko Malagarasi, daraja la Nyerere la Kigamboni na akiwa Mtendaji Mkuu wa TANROADS alisaidia ujenzi wa madaraja 1,400 Tanzania.

Pia amebuni na kusimamia barabara za kitaifa zenye urefu wa takribani kilomita 36,258.

Mhandisi Mfugale amehusika katika uchoraji mchoro wa Daraja la Kijazi lililopo Ubungo ambalo Februari 24, mwaka huu, lilizinduliwa na Hayati Rais John Magufuli na Daraja la Juu la Mfugale (Mfugale flyover) lililoko TAZARA, makutano ya barabara za Nyerere na Mandela, Dar es Salaam.

Wakati wa uzinduzi wa Daraja la Kijazi, Ubungo, Rais John Magufuli aliomba Mhandisi Mgufale asife mapema aendelee kuchora michoro ya madaraja mengine ili Dar es Salaam ibadilike.

**WASIFU WAKE**

Mhandisi Mfugale alizaliwa katika eneo la Ifunda huko Iringa, alipata elimu yake ya msingi katika Shule ya Consalata Fathers mjini Iringa na mwaka 1975 alimaliza masomo yake katika Shule ya Sekondari ya Moshi.

Mwaka 1977 aliajiriwa katika Wizara ya Ujenzi na mwaka 1983 alipata shahada yake ya kwanza Chuo Kikuu cha Rocky nchini India na ilipofika mwaka 1991 alisajiliwa kama Mhandisi Mtaalamu.

Mwaka 1992 aliteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Barabara za Mikoa na mwaka 1994/95 alipata shahada yake ya pili katika Chuo Kikuu cha Loughborough, Braunshweig nchini Uingereza na mwaka 2003 alipokea tuzo ya Distinguished Engineering Accomplishment.

Aliteuliwa kuwa Mhandisi Mkuu wa madaraja nchini Tanzania wakati huo huo na akiwa masomoni nchini Uingereza mwaka 1995 alitafiti na kutengeneza mfumo wa madaraja nchini.

Alitengeneza mfumo wa usimamizi wa madaraja kwa jina la Tanzania Bridge Management System na mwaka 2014 alisajiliwa kuwa Mhandisi Mshauri na kuwa mwanachama wa Chama cha Wahandisi Tanzania.

Nafasi nyingine alizokuwa nazo ni Mwenyekiti wa Kikosi cha Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) inayoendelea kujengwa, mjumbe wa timu ya majadiliano ya miradi mikubwa ya umeme na mwaka 2018 alipewa tuzo ya uhandisi (Engineering Excellency).

HABARI KITAIFA

# Wafungwa kuzoa taka majumbani

**Na Kulwa Mzee**

MKUU wa Gereza la Ukonga na Kamati ya Mtaa wa Kivule kwa niaba ya Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, wameingia mkataba wa miezi sita wa uzoaji taka kwa kutumia wafungwa na tayari utekelezaji umeanza.

Akizungumzia uzoaji taka katika kaya zaidi ya 8,000 Kivule, Mwenyekiti wa Mtaa, Amos Hangaya, alisema mazingira machafu yaliwalazimu kutafuta taasisi yenye uwezo na vifaa vya kufanya kazi hiyo.

Alisema kwa kushirikiana na kamati walifanya mazungumzo na Mkuu wa Magereza Ukonga, Hamisi Lissu, kuona kama wanaweza kufanya kazi ya uzoaji taka, walikubaliana ndipo Magereza walipowasilisha barua rasmi ya kuomba zabuni hiyo.

"Kamati ilijadili barua ya Magereza na kukubali kuwapa kazi hiyo kwa muda wa miezi sita na endapo watafanya vizuri tutawapeleka Manispaa kwa ajili ya utambuzi rasmi," alisema.

Amos alionyesha mkataba walioingia na Magereza Mei 11, mwaka huu na mtoa kazi ya uzoaji taka katika mkataba huo anatambulika ni Kamati ya Mtaa wa Kivule kwa niaba ya Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam na mkandararasi wa kuzoa taka ni Mkuu wa Gereza Ukonga.

Kwa mujibu wa mkataba huo mkandarasi atakuwa chini ya Ofisa Afya kwa uangalizi wa miezi sita, atatumia sheria ndogo za usafi wa mazingira za mwaka 2018, Mkurugenzi hata husika na madai yoyote ya wananchi kushindwa kulipia huduma hiyo na anaweza kuuvunja mkataba huo kwa manufaa ya umma.

Mkataba umesainiwa na Amos Hangaya, kwa niaba ya Kamati ya Kivule na Mkuu wa Gereza la Ukonga, Hamisi Lissu na shahidi Josephat Kanyamgenge ambaye ni Mkuu wa Miradi Gereza la Ukonga.

Akizungumzia ulipaji wa huduma hiyo, Amos alisema makadirio ni kaya zaidi ya kaya 8,000 zinazotakiwa kupata huduma hiyo na kila kaya inatakiwa kulipa Sh. 3,000, maduka Sh. 5,000, baa na gesti Sh. 10,000 kwa mwezi.

Alisema kuingia kwa wafungwa kuzoa taka kumeweza kuleta faida kubwa, wanazoa kila siku na kuzipeleka dampo, maeneo yamekuwa masafi ukilinganisha na siku za nyuma ambazo taka zilikuwa zinazolewa na kutupwa mitaani.

"Magereza Ukonga wametuahidi kujaza vifusi katika barabara ambazo hazipitiki, wanaanza mchakato wa kutunza mazingira, wanatarajia kuleta miche ya miti ipandwe maeneo mbalimbali," alisema.

Alisema taka zinazolewa kila siku sababu maeneo makubwa na kwamba awali walikutana na changamoto ya wananchi kugomea kulipa gharama hizo, lakini sasa hivi wameelewa.

Changamoto nyingine kwa baadhi ya kaya walikuwa hawaachi taarifa kwa watu wanaobakia nyumbani hivyo walikuwa wakifika kuzoa taka hawafunguliwi mageti.

Amos alisema changamoto hizo kwa sasa hazipo, kazi inafanyika vizuri, ratiba ya idadi ya wafungwa wangapi wanakuja kuzoa taka hiyo wanapanga wenyewe Magereza.



Mkurugenzi Mtendaji wa ITV/Radio One, Joyce Mhavile, akikabidhi zawadi kwa aliyekuwa mfanyakazi na chombo hicho, Abdallah Mwaipaya baada ya kuteuliwa na Rais kuwa Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, katika hafla fupi ya kumuaga iliyofanyika Mikocheni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Aua mke naye ajiua, mwingine akamatwa tuhuma za mauaji

**Na Wandishi Wetu, RUVUMA**

WATU wanne wamefariki dunia katika matukio mawili tofauti, likiwamo la mume kumuua mke kisha naye kujinyonga kwa kamba ya mti.

Limo pia la kuuawa kwa mtu aliyemuua Ofisa mstaafu wa Utamaduni wa Wilaya ya Mbunga, mkoani Ruvuma na kumzika ndani ya nyumba yake.

Mtu huyo aliyemua ofisa huyo naye aliuawa na wananchi wenye hasira kali, baada ya kufanya tukio jingine la wizi katika kijiji cha Liuli, wilayani Nyasa.

Tukio la kwanza lilitokea Kijiji cha Msinjili Kata ya Mlingoti Mashariki wilayani Tunduru, na kuthibitishwa na Kamanda wa Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, ambaye alisema wanaendelea na uchunguzi.

Alisema Adamu Selema (46) alifariki dunia kwa kujinyonga baada ya kumuua mkewe, Mwanabibi Mohammed (41), huku chanzo kikiwa ni wivu wa mapenzi.

Alisema tukio hilo lilitokea Juni 28, mwaka huu majira ya saa 2:00 usiku kwa kile kilichoelezwa ni ugomvi kati yao kwa mume kumshambulia mke kwa kitu kizito kwenye paji la uso kisha naye kujifunga kamba ya mti na kujining'iniza kwenye mti wa mkorosho.

Mganga aliyeufanyia uchunguzi mwili wa Mohammed, Dk. Athuman Mkonoumo, alisema chanzo cha vifo hivyo ni kubanwa mfumo wa hewa.

Wakati huo huo, Mtu mmoja Steven Hyera (50), mkazi wa Mtaa wa Bethrehemu, Mbinga Mjini, anayesadikiwa kuwa ni jambazi, ameuawa na wananchi wenye hasira kali, huku akidaiwa kuhusika na mauaji na kumzika ndani ya nyumba yake, Ofisa mstaafu wa Utamaduni wa Wilaya ya Mbinga. Ditrick Mahundi (76).

Kamanda Maigwa alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa lilitokea Juni 25, mwaka huu, majira ya 12:30 asubuhi katika kijiji cha Liuli wilayani Nyasa, na alitenda tukio hilo Juni 7, mwaka huu.

Aidha, alisema mtuhumiwa huyo alikuwa anatafutwa kwa kosa la mauaji baada ya kumuua kwa kumkatakata sehemu mbalimbali za mwili, kisha kuchimba shimo kwenye moja ya chumba cha nyumba ya Mahundi baada ya tukio hilo alikimbia na kutokomea kusikojulikana.

Kwa mujibu wa Maingwa, mtuhumiwa Hyera baada ya kufanya tukio hilo alitorokea kijiji cha Liuli wilayani Nyasa na Juni 26, mwaka huu, alikamatwa katika kijiji cha Kihagara wilayani humo kwa tuhuma za wizi na kwamba watu wenye hasira walimshambulia kwa silaha za jadi na kumjeruhi vibaya.

Kamanda Maigwa alisema walimchukua mtuhumiwa huyo na alifariki dunia baada ya kufikishwa hospitalini kwa ajili ya matibabu.

***Imeandikwa: Stevie Chindiye (Tunduru) na Gideon Mwakanosya (Songea)***

# Rais Samia aikosha NEC

**Na Godfrey Mushi, DODOMA**

HALMASHAURI Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (NEC), imempongeza kwa maandishi Rais Samia Suluhu Hassan, kwa namna alivyoendesha serikali katika siku 100 za utawala wake, akizingatia misingi ya uadilifu, haki, utawala bora na ustawi wa demokrasia.

Taarifa iliyotolewa jana na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Taifa, Shaka Hamdu Shaka, ilieleza kuwa pia katika kikao hicho, Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia, aliwataka wajumbe wa NEC kusimamia utekelezaji wa ilani ya Uchaguzi ya CCM na kupaza sauti pale ambapo wanabaini uzembe katika baadhi ya miradi inayotekelezwa na serikali.

Kwa mujibu wa Shaka, Rais Samia amesimama imara katika kusimamia umoja wa kitaifa na mshikamano kwa wananchi.

"Wajumbe wa NEC wametoa pongezi kwa Rais Samia na pia wameazimia pongezi hizo apatiwe kwa maandishi kwa namna alivyoweza kupokea madaraka makubwa ya nchi na kulivusha taifa salama wakati taifa lilipoondokewa na Rais Dk. John Magufuli.

"Serikali yake imeendelea kuwajali wananchi wa chini kupitia bajeti, ambayo asilimia 90 imegusa wananchi."

Kwa mujibu wa Shaka, wajumbe wa NEC walisema bajeti hiyo ya mwaka 2021/2022, imetoa dira na mwelekeo wa kupambana dhidi ya umaskini na ukali wa maisha.

Aidha, Shaka alisema Rais Samia aliwakumbusha wajumbe hao kwamba wana wajibu wa kusimamia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM katika maeneo yao.

Alisema wajumbe hao wanapaswa kutekeleza wajibu huo bila uoga na wasisite kupaza sauti pale wanapobaini baadhi ya miradi utekelezaji wake hauendi kama ilivyokusudiwa.

Vile vile, Shaka alisema NEC ilimpongeza pia Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa kutekeleza ilani ya uchaguzi ya CCM kwa kuzingatia maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Alisema katika uongozi wa Rais Dk. Mwinyi, milango ya kiuchumi imeendelea kufunguka, ambapo amekuwa akipokea wawekezaji na watu mashuhuri wenye nia ya kutaka kuwekeza kupitia uchumi wa buluu.

## HABARI KITAIFA

# Mwaipaya apewa mbinu utekelezaji majukumu

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro, Abdallah Mwaipaya, ametakiwa kuwa mtu wa vitendo zaidi na kupokea ushauri katika utekelezaji wa majukumu yake.

Ushauri huo ulitolewa jana Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa ITV na Radio One, Joyce Mhavile, wakati wa hafla ya kumpongeza na kumuaga mtangazaji huyo kutokana na uteuzi uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni.

Hafla fupi ya kumuaga iliandaliwa na Kituo cha Televisheni cha ITV alichokuwa akifanya kazi kabla ya kuteuliwa na aliahidi kushirikiana na wananchi katika kutatua changamoto zinazowakabili.

Mhavile alimtaka Mwaipaya wakati akitimiza majukumu yake kuwa mtu wa utekelezaji badala ya kuahidi na kumtaka awe na utaratibu wa kusikiliza ushauri wa watu ili kumsaidia katika kazi zake.

"Kiongozi mzuri ni yule anayesikiliza maono na ushauri wa wananchi wake. Mwananchi anapokuja kukueleza changamoto unampa nafasi aeleze mtazamo wake. Ukishafanya hivyo naamini mtu yeyote au kiongozi atakayekuja kwako watakuja na suluhisho.

"Pia kiongozi mzuri ni yule msikivu ili apate matokeo chanya na usipofanya hivyo ni kama alivyosema Rais kuwa mkinizingua tutazinguana. Nakutakia kila la heri unapokwenda kutekeleza majukumu uliyopangiwa," alisema.

Mwaipaya kwa upande wake alimshukuru Rais Samia kwa kumwamini na kumteua katika nafasi hiyo na amemwahidi kuwa atatekeleza majukumu yake ipasavyo na hatamwangusha.

Alisema anaamini kuwa kwa kushirikiana na wasaidizi wake watafanya kazi kwa weledi ili kuhakikisha kuwa wanaleta maendeleo katika wilaya yake na taifa kwa ujumla.

"Naushukuru pia uongozi wa ITV kwa kunipokea na kufanya kazi na mimi kwa zaidi ya miaka 20. Naamini kujituma na kufanya kazi kwa bidii ndiyo sababu nimeonekana, hivyo naamini tutashirikiana katika kuleta maendeleo ya taifa letu," alisema.


**UBALOZI WA MAREKANI, SWEDEN, NETHERLANDS, DENMARK, UNICEF WORLD BANK GROUP & R I LTD DAR ES SALAAM**

**MNADA WA HADHARA:**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa Marekani na Balozi zingine tajwa hapo juu watauza kwa mnada wa hadhara Funicha za nyumbani, Piki piki, Genereta na Magari tarehe 3 July, 2021 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

Fenicha na Computer zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi: Sofa set, China base, Hutch, Chest drawer, Dresser, Credenza, Dining table, Book case, Study desk, Chairs, Carpet, Vitanda, Magodoro, Fridge double door, Freezer, Washer, Dryer, electric cooker, A/c split units, Canon Photocopy , TV set, Computer set, Colour Printers, Health Massage Chair na vingine vingi.

**Magari yataanza kuuzwa kuanzia saa 6:00 mchana:**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota RAV4 Station Wagon | VVT- I Petrol Engine | 2006 | Haujalipwa |
| 1 | Toyota Land Cruiser Prado | VZJ12 Petrol Engine | 2004 | Haujalipwa |
| 1 | Nissan X-Trail Station Wagon | NT32 Petrol Engine | 2014 | Haujalipwa |
| 4 | Honda Motorcycle CTX200, CRF250R | XL125S Petrol Engine | 2006,2013 | Haujalipwa |
| 2 | Yamaha Motorcycle YBR125G | Petrol Engine | 2016 | Haujalipwa |
| 1 | Genereta 27 Kva 3 Phase | Perkins Engine Diesel | - | Haujalipwa |
| 1 | Hyster Fork Lift 3Tons | Perkins Engine Diesel | 1998 | Haujalipwa |
| 4 | Canon Photocopy Machine | C222i and IR202i Color | - | Haujalipwa |
| 2 | Xerox work centre 7970 | Kyocera 250Ci | - | Haujalipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 30 Juni mpaka 2 July, 2021, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

216336601

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari, Fork Lift na Genereta atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 4 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 9 July, 2021 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya VISA na Master cards za CRDB na NBC yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini na kuwa na barakoa.

For further information contact:
UNIVERSAL AUCTION CENTRE,
(PLOT NO. 5 "E" LION STREET SINZA)
CELL NO: 0754 284 926
Insta: universalauctioncentre

DAR ES SALAAM
E-mail: universalauction@hotmail.com





Wafanyabiashara wakiingiza bidhaa zao kwenye banda kwa ajili ya maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, Uwanja wa Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Samia ataka Watanzania kuendelea kuchapa kazi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema anaridhika na mafanikio yaliyopatikana katika siku 100 za urais na kuwataka Watanzania kutoridhika na kuendelea kuchapa kazi mara mbili ya sasa.

"Wanawake na wanaume twendeni tukafanyekazi pale tulipo, tujenge taifa letu," amesisitiza.

Alisema hayo juzi, wakati alipokutana na wahariri na waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari nchini, Ikulu, jijini Dar es Salaam.

Tangu alipoapishwa rasmi kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Machi 19, 2021, baada ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, John Magufuli, Rais Samia amejiwekea utaratibu wa kukutana na makundi mbalimbali nchini.

Katika kipindi cha siku 100 alichokaa Ikulu, Rais Samia ameshakutana na makundi kadhaa likiwamo kundi la Wazee, Bunge, Wanawake, Viongozi wa Dini, Vijana, Viongozi wa Kanisa Katoliki (TEC) na Wanahabari.

Rais Samia alisema lengo la kukaa na makundi hayo ni kuwasikiliza na kujifunza kutoka kwao na kuwashukuru Watanzania kwa kumpa moyo, ari na nguvu.

Alisema kupitia maoni mbalimbali anayoyapata katika siku zake 100 anafarijika hatua anazozichukua kupokelewa vizuri na wananchi.

"Naridhika na mafanikio yaliyopatikana, lakini tusiridhike na haya tuliyopata, twendeni tukafanye kazi mara mbili na tunayofanya sasa hivi."

"Kazi ya urais ni ngumu, lakini kwa sababu ni taasisi inashirikiana na vyombo vingine hapo ndipo unapokuja urahisi wake. Si rahisi kihivyo kuna ugumu wake ni lazima kila siku ujue kila kitu kinachoendelea nchini."

Rais Samia alisema anajivunia Tanzania kuhimili vishindo vya kuteremka kwa uchumi na thamani ya fedha kuendelea kuwa imara na kuwa na akiba ya chakula cha kutosha.

"Mpaka sasa tupo stable (imara) na tunakwenda vizuri nina imani tutakwenda vizuri," alisema.

# Aveva asema kamati iliamua Hans Pope alipwe $ 17,000

**Na Hellen Mwango**

RAIS wa zamani wa Klabu ya Simba, Evans Aveva, amedai mahakamani kuwa kamati tendaji iliamua zitumike Dola za Marekani 17,000 kati ya Dola 319,212 kulipwa aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili, Zachariah Hans Pope alizokuwa akiidai klabu hiyo.

Kadhalika, alidai kuwa akiwa rais 2014 mpaka 2017 ndani ya muda huo, klabu ilipata Dola 319,212 baada ya mauzo ya mchezaji, Emmanuel Okwi, kwenda klabu ya Etoile du Sahel ya Tunisia, aliitisha kikao cha kamati tendaji kuzungumzia matumizi ya fedha hizo.

Aveva alitoa madai hayo jana wakati akitoa ushahidi wake wa utetezi dhidi ya kesi kula njama na matumizi mabaya ya madaraka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Aveva ambaye ni shahidi wa kwanza wa utetezi, alitoa ushahidi wake wakati akiongozwa na Wakili wa Utetezi, Kung'he Wabeya.

"Katika kikao hicho, kamati iliamuru matumizi ya fedha hizo na kwamba zitumike katika ujenzi wa uwanja wa klabu Bunju na Dola 17,000 kati ya Dola 319,212 alipwe aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili, Zachariah Hans Pope, alizokuwa akiidai klabu yetu," alidai.

Alidai sekretarieti ya klabu ilipendekeza fedha hizo ziwekwe katika akaunti maalum na hivyo ukafanyika mchakato wa kufungua akaunti nyingine.

Aveva alidai kuwa ufunguaji wa akaunti hiyo ulishindikana, lakini aliombwa fedha hizo zihamishiwe katika akaunti yake binafsi.

"Nilipoombwa kuzihifadhi fedha hizo kwenye akaunti yangu binafsi wakati tunaendelea na mchakato wa kufungua akaunti ya klabu, kama kiongozi mkuu wa klabu nilikubaliana na ombi hilo, lakini nilitoa sharti kwamba lazima kuandaliwe memorandum kuhusu suala hilo, iliandaliwa na ikasainiwa na watu watatu ambao ni mimi rais wa klabu, Makamu wa rais, Geofley Nyange maarufu kama Kaburu na Katibu Mkuu ambaye alikuwa Mhasibu wa klabu, Amos Gaumeni," alidai Aveva.

Akifafanua, alidai baada ya kuandaliwa kwa mkataba huo wa makubaliano uhamishaji fedha ulianza katika Benki ya CRDB.

Alidai pia kuhusika kwenda benki kusaini fomu ya kuhamisha fedha hizo na Gaumeni alikamilisha taratibu za kibenki kuhamisha fedha hizo. Kesi hiyo itaendelea kusikilizwa Julai 12, mwaka huu.

Katika kesi ya msingi, Aveva na Kaburu wanadaiwa kula njama ya kutenda kosa la matumizi mabaya ya madaraka.

Pia wanadaiwa kutumia vibaya madaraka yao kwa kuandaa fomu ya kuhamisha fedha Dola za Kimarekani 300,000 kutoka kwenye akaunti ya Simba iliyoko benki ya CRDB Azikiwe kwenda kwenye akaunti binafsi ya Aveva iliyoko benki ya Barclays.

# PSSSF yaanika utaratibu wa mikopo ya nyumba

**Na Elizabeth Zaya**

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) umesema umedhamiria kwa dhati kuhakikisha unawawezesha wanachama wake na wananchi kwa ujumla kumiliki nyumba na viwanja sehemu mbalimbali nchini kwa kulipa kidogokidogo.

Hayo yalibainishwa na Meneja Uhusiano wa Mfuko huo, James Mlowe, alipokuwa akizungumza kwenye banda namba 13 la mfuko huo kwenye Viwanja vya Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam.

Alisema PSSSF inawaalika wanachama wake na wananchi kwa ujumla kutembelea banda lake ili kupata taarifa za huduma mbalimbali zikiwamo zile la kumiliki nyumba kwa gharama nafuu.

"Tumeingia makubaliano na Benki ya Azania ambayo itawawezesha wanachama na wananchi kukopa mikopo ya makazi (Mortgage loan) kwa masharti nafuu ili kununua nyumba na viwanja vinavyomilikiwa na PSSSF kupitia uwekezaji iliyoweka sehemu mbalimbali nchini kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Shinyanga, Tabora, Mtwara na Iringa na mradi wa viwanja vya gharama nafuu ... viko katika mikoa ya Ruvuma, Kagera, Tabora, Iringa, Katavi, Morogoro, Dar es Salaam, Rukwa, Lindi na Mtwara," alisema.

Akifafanua kuhusu masharti ya kukopa nyumba na viwanja, Mlowe alisema, mteja atalazimika kuweka rehani ya asilimia 10 ya thamani ya mkopo au mali ya thamani hiyo kwa dhamana ya mkopo na kiwango cha juu kabisa ambacho mteja anaweza kukopeshwa na benki ni asilimia 90 ya thamani yote ya nyumba au kiwanja.

"Mteja atakapokamilisha malipo yake atakabidhiwa hati yake ya nyumba au kiwanja na Benki ya Azania na muda wa marejesho ya mkopo ni kipindi kisichozidi miaka 15 kwa mkopo wa nyumba na miaka miwili kwa mkopo wa kiwanja," alifafanua Mlowe.

Kuhusu huduma nyingine ambazo wananchi na wanachama watafaidika kwa kutembelea banda hilo ni wanachama kupata taarifa za michango, uwekezaji, mafao ya uzazi, pensheni ya uzeeni, Pensheni ya Warithi, Pensheni ya Ulemavu.

**"Tumeingia makubaliano na Benki ya Azania ambayo itawawezesha wanachama na wananchi kukopa mikopo ya makazi (Mortgage loan) kwa masharti nafuu ili kununua nyumba na viwanja vinavyomilikiwa na PSSSF kupitia uwekezaji iliyoweka sehemu mbalimbali nchini kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Shinyanga, Tabora, Mtwara na Iringa na mradi wa viwanja vya gharama nafuu ... viko katika mikoa ya Ruvuma, Kagera, Tabora, Iringa, Katavi, Morogoro, Dar es Salaam, Rukwa, Lindi na Mtwara," alisema.**



Meneja Uhusiano wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), James Mlowe (kulia), akizungumza na mwanachama wa mfuko huo, Philipo John alipotembelea banda la PSSSF kwenye maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, Uwanja wa Mwalimu Nyerere Barabara ya Kilwa jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# UDART yabainisha vikwazo uendeshaji

**Na Maulid Mmbaga**

MKURUGENZI Mtendaji wa Mabasi ya Mwendokasi (UDART), John Nguya, amebainisha vikwazo vinavyoikabili wakati wa utekelezaji wa majukumu yake ikiwamo uhaba wa mabasi jambo linalosababisha abiria kubanana na wengine kukaa muda mrefu kituoni wakisubiria usafiri.

Aliyasema hayo jana Jangwani jijini Dar es Salaam huku akibainisha kuwa kikwazo kingine ni bodaboda na magari yanayopita katika njia ya mwendokasi, hivyo kuwa chanzo cha ajali.

Nguya alitaja tatizo lingine kuwa ni wafanyabiashara wanaofanya kazi zao karibu na barabara ya mwendokasi katika maeneo ya Msimbazi na Kivukoni jambo ambalo ni hatari kwa usalama wao.

"Mimi naamini kuwa tunaweza kuwatafutia sehemu nzuri na wao wakaridhika ili kuepusha madhara ambayo yanatokana na ajali za mara kwa mara kati ya magari yetu na wafanyabiashara wa maeneo hayo," alisema Nguya.

Aliongeza kuwa katika jitihada za kutatua matatizo hayo, wamepokea mabasi mapya 70 na wanatarajia yatapunguza tatizo la usafiri kwa kiasi kikubwa hasa abiria kukaa kituoni kwa muda mrefu na kujazana kupita kiasi.

"Tuna imani na mkuu wa mkoa, hivyo tunaomba hizi changamoto (matatizo) ambazo (ambayo) ziko (yako) chini yake kama kulinda barabara zetu na tunaomba tushirikiane kuzitatua," alisema.

UDART ilianza kazi ya zabuni ya kusafirisha abiria wa mkoa huo Mei 16, 2016 na mpaka sasa mradi huo uko katika majaribio na katika hatua hiyo, alisema wamepata mafanikio ikiwamo kupunguza adha ya usafiri kwa kuwa wamekuwa wakisafirisha abiria kati ya 80,000 hadi 240,000 kila siku.

Mafanikio mengine ni kutoa ajira kwa watu takribani 800 na idadi hiyo itaongezeka pindi mabasi hayo 70 waliyoyapokea yatakapoanza kazi, kuleta ustaarabu katika usafiri wa mijini kwani mabasi hayo yanazingatia viwango vya kimataifa.

"Jambo lingine ni kuleta tija katika uzalishaji wa taifa letu kwa kuwawahisha wananchi katika majukumu yao, kwa mfano kutoka Kivukoni mpaka Kimara zamani tulitumia masaa matatu na zaidi lakini sasa kwa usafiri huu tunatumia dakika 35, na hatujawahi kukosa kutoa huduma kwa sababu yeyote, iwe mvua iwe jua tuko kazini," alisema.

# Manispaa yavunja uzio nyumba ya mwasisi wa TANU na CCM

**Na Richard Makore, MWANZA**

HALMASHAURI ya Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza imevunja uzio wa nyumba ya aliyekuwa mwasisi wa Chama cha TANU na Chama Cha Mapinduzi (CCM), William Kafiti.

Uzio huo pamoja na nyumba vina hati namba 1825 kitalu C Buswelu iliyotolewa mwaka 2016.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi nyumbani kwa marehemu Kafiti, mtoto wa mwasisi huyo, Mapuli Kafiti, alisema hawakupewa taarifa ya kuvunja ukuta huo ingawa awali ilikuwapo taarifa ya kuomba kuonyeshwa mipaka ya eneo hilo.

Mapuli alisema ukuta huo ulivunjwa pamoja fremu za maduka mawili yaliyokuwa na mali za wapangaji zinazofikia thamani ya Sh. milioni 7.7.

Alisema wanaona kama wamewaonea kwa kuwa kuna hatimiliki ya eneo hilo na majengo mapya kwa zaidi ya miaka saba huku uzio ukiwapo kwa zaidi ya miaka 30.

"Nakumbuka Aprili 22 ililetwa barua ikielekezwa kwa William Kafiti ambaye ni marehemu ikimtaka avunje eneo hili. Lakini kwa nini halmashauri ivunje eneo lenye hati?" Alihoji.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, John Wanga, amekiri kuvunjwa kwa ukuta huo na kueleza kuwa umejengwa eneo ambalo itapita barabara ya mtaa.

"Ni kweli ukuta umevunjwa ili kupanua sehemu ya barabara ya mtaa kwa kuwa ukuta huo ulikuwa umeingia ndani mita chache," alisema.


bgtl

BEST GROUP (T) LIMITED

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa Idhini tuliyopewa na BANK OF AFRICA TANZANIA LIMITED Tutauza kwa MNADA WA HADHARA baadhi ya vifaa mbalimbali vya BENKI hiyo vilivyotumika. Mnada utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 03/07/2021 kuanzia saa 3:00 asubuhi na kuendelea.

| Na. | MAELEZO YA VITU VYA MNADA | MAHALI |
|---|---|---|
| 1 | i. Majenereta, Sanduku za kutunzia fedha, ATM na vifaa mbalimbali vya ofisini<br>ii. NISSAN PICKUP VP DOUBLE CABIN X/38/2021<br>iii. LAND ROVER FREELANDER STATION WAGON (5 DOOR)2009 | Kiwanja Na. 38 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi Mkabala na Ubalozi wa Ufaransa. |

MASHARTI YA MNADA

1. Mali zitauzwa kama zilivyo
2. Ukaguzi ni kuanzia tarehe 01/07/2021 hadi 02/07/2021 kuanzia saa 3:00 asubuhi mpaka saa 10:00 jioni, barabara ya Ali Hassani Mwinyi, kiwanja na. 38 mkabala na ubalozi wa Ufaransa.
3. Kiingilio ni Tsh.20,000/= kwa mtu mmoja na wafanyakazi wa benki wataingia na vitambulisho vya ofisi.
4. Mali zitakazo nunuliwa kwa bei ya kuanzia milioni kumi (10,000,000/=) kushuka chini zitalipwa kwa asilimia mia moja(100%) na mali zitakazouzwa kwa zaidi ya milioni kumi(10,000,000/=) zitalipwa malipo ya asilimia ishirini na tano(25%) na kiasi kilichobaki asilimia sabini na tano(75%) kitalipwa ndani ya siku tatu za kazi, kushindwa kufanya hivyo kiasi kilicholipwa awali hakitarudishwa na mali hiyo itauzwa kwa mshindi wa pili.
5. Mali zilizonunuliwa zitatakiwa kuondoshwa eneo la mnada ndani ya siku tatu za kazi baada ya malipo ya asilimia mia moja (100%) na kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atatakiwa kulipia gharama za utunzaji wa mali hizo.

216336102

Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi Mtendaji
Best Group (T) Ltd
Alli Hassan Mwinyi Road
Green Acres Buliding, 2nd Floor
P.O. BOX 1088
Dar Es Salaam.
Mob: + 255 715-363537/ +255 765-363537

AU

Mkurugenzi Mtendaji
BANK OF AFRICA
Head Office,
NDC Development House, Ohio street / Kivukoni
P.O. BOX 3054,
Dar Es Salaam, Tanzania.
Tel: +255 22 2214000

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watanzania tuchangamkie fursa eneo huru la biashara

JUZI Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Leberata Mulamula, alisema serikali imekamilisha mambo yote ya msingi yanayotakiwa kuwa kwenye mkataba wa biashara kwa nchi za Afrika na sasa serikali itaridhia.

Nchi nyingi za Afrika zimesharidhia mkataba huo mwaka 2018 na utekelezaji ulianza mwaka 2019, lakini Tanzania ilibaki nyuma kwa mwaka mmoja.

Waziri alikutana na Katibu Mtendaji wa Eneo huru la Biashara la Afrika (AfCFTA), Wamkele Mene, na kumhakikishia kuwa Tanzania imeshakamilisha kila kinachotakiwa na iko tayari kuridhia na kusaini mkataba huo kwa manufaa ya watu wake.

Hii ni habari njema kwa kila Mtanzania kwa kuwa faida ya kuridhia mkataba huo ni uhakika wa soko kubwa la zaidi ya watu bilioni moja kwa kuuza na kununua bidhaa bila vikwazo, na sasa ni wakati wa Watanzania kwa nyakati na nafasi tofauti kuchangamkia fursa zote muhimu.

Huu siyo mkataba wa kwanza kwa Tanzania kuridhia katika eneo la biashara, ipo mingi ikiwamo mkataba wa mpango wa soko la AGOA (African Growth and Opportunity Act).

Katika bajeti ya mwaka huu, serikali ilieleza kuwa nchi imeendelea kunufaika na Mpango wa AGOA kwa kuruhusiwa kupeleka zaidi ya bidhaa 6,400 bila kulipa ushuru wa forodha.

Aidha, katika kutekeleza mkakati wa kitaifa wa AGOA, Wizara ya Viwanda na Biashara imeendelea kuhamasisha wafanyabiashara wa Tanzania kuwekeza, kutumia ipasavyo fursa za soko hilo ili kukuza mauzo ya bidhaa zetu, kuongeza fedha za kigeni, kuchochea ukuaji wa viwanda pamoja na kukuza ajira nchini.

Sasa imekuja fursa ya eneo huru la biashara, ni wakati wa Watanzania kuuza mazao na bidhaa mbalimbali zinazozalishwa nchini na kuwa na utambulisho wa nchi yetu.

Ni muhimu katika hili changamoto zote zikatatuliwa na kubwa ni vifungashio ambavyo hutumika vya nje ya nchi, jambo ambalo linaitambulisha nchi husika ilhali bidhaa zinazalishwa Tanzania.

Mathalani, wakati wa Bunge la Bajeti, wabunge kutoka maeneo yanayolima maparachichi ya kisasa walisema kuna nchi jirani inauza vifungashio na wakati mwingine wanachukua bidhaa nchini na kwenda kuzipakia kwenye vifungashio hivyo na kusafisha katika masoko ya Ulaya, Marekani na Uarabuni na kuonyesha bidhaa hiyo imetoka nchi hiyo.

Hili si jambo dogo ni salamu kuwa sasa nchi iwe na mpango wa kuzalisha vifungashio vyake vya kuitambulisha kokote kulingana na bidhaa husika ili kuendelea kutambulisha bidhaa zetu zenye ubora.

Lakini wakati hilo likifanyiwa kazi, ni wajibu wa Wizara ya Kilimo kuhakikisha wanatoa elimu kwa wakulima kuzalisha kwa ubora na huduma zote muhimu za ugani.

Katika soko la ushindani kinachokubeba ni bidhaa bora na siyo jina la nchi yako, kama utaweza kuzalisha bidhaa na mazao bora maana yake utajitangaza duniani.

Tunaona ni muhimu sana kwa Wizara za Viwanda kushirikiana kwa karibu katika kuhakikisha bidhaa na mazao yanayolepekwa nje ziwe na ubora unaotakiwa, na hili litafanikiwa ikiwa huduma za ugani zitatolewa kikamilifu ikiwamo kuwezesha wajasiriamali kufikia fursa hizo.

Pamoja na jihitaha za serikali pia ni wajibu wa sekta binafsi kupitia Jumuiya ya Wafanyabiashara na wajasiriamali nchini kuchangamkia kikamilifu fursa hiyo na sasa bidhaa za Tanzania ziendelee kuuzwa nchi za Afrika, na kuliwezesha taifa kupata fedha za kigeni na ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# 'Vyama vya upinzani subira yavuta heri'

Na Sabato Kasika

LEO Rais Samia Suluhu Hassan, anatimiza siku 104 tangu aanze kuongoza serikali ya awamu ya sita kazi iliyoanza Machi mwaka huu.

Amefanya mambo mengi kwa ajili ya ustawi wa taifa yakihusisha uteuzi wa watendaji na viongozi unaozingatia uwiano wa kijinsia.

Wataalamu wa sayansi ya siasa na utawala bora, wana msemo usemao kila serikali mpya inapoingia madarakani inakuwa na mtaji wake.

Msemo huo unamaanisha kila utawala mpya unapoingia madarakani, hupenda kufanya kazi na aina ya viongozi unaowataka. Wapo wa kuteuliwa upya au kuchagua miongoni mwa waliokuwa katika serikali iliyomaliza muda wake.

Hivyo ndivyo imekuwa ikifanyika hata hapa nchini, ambapo Rais Samia, aliyerithi nafasi ya urais baada ya kifo cha mtangulizi wake, hayati Dk. John Magufuli, akiwa leo ametimiza takribani miezi mitatu na nusu.

Rais anabainisha kuwa katika uwaziri kuna asilimia 20, wakuu wa mikoa asilimia karibu 30 na maofisa tawala wa mikoa (RAS) hadi asilimia 45 hadi 46, wakuu wa wilaya asilimia 44, na anakaribia asilimia 50 kama yanavyoelekeza Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs).

Katika uteuzi huo anaweka wazi kuwa unazingatia sekta binafsi ikiwamo vyombo vya habari, taasisi na vyama vya siasa, na kwamba juhudi zinafanyika kwa wanawake kuchukua nafasi zaidi ya uongozi kwenye bodi za wakurugenzi kwenye mashirika.

Lakini, pia Rais anaweka wazi kuwa, uteuzi wa vijana ni zaidi na amelenga vijana wanaoweza kufanya kazi kuchangia maslahi ya taifa, bila kuwa ni wa upinzani, vyombo habari, hata wale wasio wanachama wa vyama vya siasa.

Hata hivyo, mara tu baada ya kuingia madarakani Machi 19, mwaka huu, viongozi wa vyama vya upinzani walimuomba kurejesha mchakato wa kupatikana katiba mpya na pia kuruhusu mikutano ya hadhara.

Baada ya maombi hayo, ameamua kutoa ufafanuzi na kuwataka Watanzania wawe na subira, kwa kuwa ameshapanga kukutana na wanasiasa na kwamba kuhusu katiba mpya, vyote vitashughulikiwa.

Anataja kipaumbele kuwa ni uchumi na kwamba kila kitu kitakaa sawa uchumi ukiimarika, hivyo anataka kujenge kwanza uchumi.

Anasema: "'Nipewe muda kusimamisha nchi kiuchumi, itafuata kushughulikia katiba mpya na kuruhusu mikutano ya hadhara. Katiba ni ya maana sana, msubiri nisimamishe nchi kiuchumi, tutakwenda katika siasa."

Kauli hiyo ya Rais inaonyesha wazi kuwa ana nia njema ya kutaka kutimiza kile ambacho vyama vya upinzani vimekuwa vikitamani, lakini jambo la muhimu ni kumpa nafasi ili ajipange kwanza kabla ya kutimiza wanachokitaka.

Hivyo si vibaya viongozi wa vyama hivyo wakaelewa nia ya Rais na kuwa na subira, kwa kuzingatia kwamba, subira huvuta heri, mvumilivu hula mbivu.

Rais ameonyesha anavyojiamini na kusimamia haki, kwani hata baadhi ya watu waliodhulumiwa haki zao wamerejeshewa, hivyo inawezekana huko ambako wapinzani wanataka, atafika, suala ni muda.

Ikumbukwe kuwa, katika kipindi kifupi ambacho ameingia madarakani, baadhi ya vyama vya siasa vimefanya ziara ya mwezi mzima bila kukumbana na dhoruba ya vyombo vya dola wala kukamatwa.

Hatua hiyo inatosha wanasiasa kutambua kuwa Rais ana nia njema kwa vyama hivyo, suala la msingi ni kuvumilia.

# Mfumo anwani za makazi kukabili uhalifu, majanga

**Na Godfrey Mushi, DODOMA**

SERIKALI imesema mpango wa utekelezaji wa anwani, postikodi na makazi unakuja na mfumo mpya wa kurahisisha kazi ya kukabiliana na majanga ya moto na uhalifu katika maeneo mbalimbali nchini.

Mpango huo ambao hadi sasa umeshatumia zaidi ya Sh. bilioni tatu, utekelezaji wake unaendelea katika Jiji la Mwanza.

Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Andrew Kundo, akizungumza jana jijini Dodoma, wakati wa kuutambulisha rasmi mfumo huo kwa wabunge maarufu 'NAPA', alisema umegawanyika katika sehemu mbili.

"Pia mfumo huu utalisaidia sana Jeshi la Polisi, kufanya kazi zake kwa urahisi zaidi, kwa sababu mfumo wetu huu wa sasa utakuwa unachukua taarifa zote nchini, barabara zote, vyombo vyote, vituo vya afya vyote, vituo vya polisi vyote na majengo yote ya serikali.

"Tunakwenda kwenye uelekeo ambao watu wengi walikuwa wakilalamika kwamba tulikuwa tunatumia mfumo wa kigeni. Mfumo huu una application (programu) ambayo inachukua taarifa zote za makazi na wakazi, biashara na maofisi."

Aidha, Kundo alisema mfumo huo, utaifanya serikali kuacha kutegemea matumizi ya mifumo ya kizamani ambayo inatumia kama Google Map.

Kuhusu mageuzi ya huduma za Posta, Naibu Waziri huyo, alisema wataalamu wa wizara hiyo wanajenga mfumo ambao hautakuwa na mianya ya taarifa za ndani za serikali kutoka nje ya nchi.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Zainab Chaula, alisema tayari wizara hiyo imeshapeleka mwongozo wa utekelezaji wa mpango huo katika kata zote 359 zilizopo nchini.

## Polisi Dar wanasa silaha, watuhumiwa 60 uhalifu

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, linawashikilia watu 60 wanaokabiliwa na tuhuma mbalimbali za uhalifu pamoja na silaha mbili ikiwamo moja iliyotelekezwa ofisi ya Posta Kariakoo.

Kamanda wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na operesheni ya kuzuia na kupambana na uhalifu inayoendelea.

"Watuhumiwa hawa walikamatwa na vielelezo mbalimbali yakiwamo magari matatu, T 730 BCT aina ya Toyota RAV4, T 677 DRJ aina ya Toyota IST naT 220 CWJ aina ya Alteza, pikipiki nne zenye namba za usajili MC 801 CNG, MC875 BUR, MC 932 CTE na MC 665 CVD ambazo ziliibwa," alisema.

Kamanda Muliro alisema watuhumiwa hao pia walikutwa na runinga aina ya LG nch 32, friji aina ya Hisence, simu tano za aina mbalimbali na kompyuta mpakato aina ya Dell.

Kuhusu silaha zilizopatikana, alisema Jumamosi iliyopita silaha aina ya Glock BUT 614 yenye namba NE 00079337 iliibwa eneo la Hospitali ya Hindu Mandal kutoka kwa Jabi Mwasha na baadaye kutelekezwa katika ofisi ya Posta tawi la Kariakoo.

Alisema silaha ya pili aina ya Glock 17 yenye namba AMP 490 ikiwa na risasi moja ilipatikana siku iliyofuata (Jumapili) vichakani eneo la Chanika Nguvukazi baada ya wananchi kutoa ushirikiano.

## Watoto wa kike walia kubaguliwa kurithi mali

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

WATOTO wa kike mkoani Shinyanga, wamelalamikia kitendo cha baadhi ya wazazi mkoani humo, kuendekeza mila kandamizi za kuwabagua na kuwanyima kurithi mali, huku wakiwathamini watoto wa kiume.

Hayo yalibainishwa juzi na watoto wa Kanisa la International Evangelical Assemblies of God Tanzania (IEAGT), la Mjini Shinyanga kwenye Wiki ya Watoto Kanisani hapo.

Alisoma risala kwa niaba ya watoto wenzake Naomi Daudi, alisema baadhi ya wazazi mkoani Shinyanga bado wanaendekeza masuala ya mfumo kandamizi kwa watoto wa kike na kushindwa kuwarithisha mali na kuwapa wa kiume peke yao.

"Kupitia wiki yetu ya watoto kanisani hapo, tunaomba kufikisha ujumbe kwa wazazi mkoani Shinyanga na Tanzania kwa ujumla, waache kuwabagua watoto wa kike kuwarithisha mali wote tune haki sawa," alisema Naomi.

Katika hatua nyingine, aliwataka wazazi kuacha migogoro ya kifamilia na wengine kugombana mbele ya watoto, hali ambayo wameeleza imekuwa ikiwaathiri watoto wengi kisaikolojia, na hata kufanya vibaya masomo yao.

Mchungaji wa Kanisa hilo, David Mabushi, aliwataka wazazi na walezi mkoani humo, kuwalea watoto wote kwa usawa na kuwapatia haki zao bila ya kujali jinsia zao.

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF WATER**

**Invitation for Bids**
**For**
**Supply of Office Furniture**

***Tender No. ME-011/2020-2021/G/34***

## Invitation for Tenders

The Government of the United Republic of Tanzania has received funds from Development Partners towards the implementation of Water Sector Support Program (WSSP II) during the financial year of 2020/2021 and it intends to apply part of the proceeds of the funds to cover eligible payments under the Contract for Supply of Office Furniture.

1. The Ministry of Water now invites sealed bids from eligible Suppliers of the following goods:

**Supply of Furniture**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Visitors Benches | 2 | 14 | Oval conference table | 1 set |
| 2 | Coffee Tables | 1 | 15 | Executive chair | 1 |
| 3 | Coffee Tables | 1 | 16 | Office Chairs | 50 |
| 4 | Office Tables | 22 | 17 | Visitor Chairs | 30 |
| 5 | Secretarial table | 2 | 18 | Conference chairs | 80 |
| 6 | Conference Tables | 4 | 19 | Confence chairs | 7 |
| 7 | Conference Tables | 40 | 20 | Secretarial chairs | 3 |
| 8 | Office Tables | 11 | 21 | Canteen Chairs | 41 |
| 9 | Canteen Tables | 10 | 22 | Library Chairs | 10 |
| 10 | Executive table | 1 | 23 | Steel cabinets | 20 |
| 11 | Executive sofa | 1 | 24 | Shelve | 10 |
| 12 | Waiting sofa | 1 | 25 | Racks | 6 |
| 13 | Mini fridge | 1 | 26 | Safe Box | 1 |

2. Bidding will be conducted through the National Competitive Bidding (NCB) procedures specified in the Public Procurement (Goods, Works, Non-Consultant Service and Disposal of Public Assets by Tender) Regulations, 2013 – Government Notice No.446 as amended and are open to all Bidders as defined in the Regulations.

3. Interested eligible Bidders may obtain further information from and inspect the Bidding Documents at the office of the Secretary, Ministerial Tender Board, Ministry of Water, P. O. Box 456, Kolon Building opposite DUWASA Head Office, PMU Office, 40473 Dodoma. Email: pmu@maji.go.tz Dodoma from 8.00 to 15:30 on Monday to Friday inclusive except on public holidays.

4. A complete set of Bidding Document(s) in English and additional sets may be purchased by interested Bidders on the submission of a written application to the address given under paragraph 6below and upon payment of a non-refundable fee of Tanzania Shillings One Hundred Thousand (TShs. 100,000.00). Payment shall be made through the electronic payment system therefore interested bidders are invited to collect the Control number for effecting the payment.

5. All Bids must be accompanied by Unconditional Bid security equivalent to 2% of the tender price in an acceptable form as provided in the bidding document. Bid Security must properly address to the following address: Permanent Secretary, Ministry of Water, P.O. Box 456, and 40473 Dodoma.

6. All sealed bids in One (1) original plus Three (3) copies, properly filled and enclosed in plain envelopes must be delivered to the address given below on 13th July 2021 before or at 11:00 hour's local time. The outer envelope of the bid should be clearly sealed and addressed to the Secretary, Ministerial Tender Board, Ministry of Water P. O. Box 456 Dodoma, and marked "TENDER NUMBER. ME/011/2020-2021/G/34 FOR SUPPLY OF OFFICE FURNITURE and Marked DO NOT OPEN BEFORE 11:00 HOURS Local Time. Bids will be opened promptly after the deadline at a public bid opening ceremony to be held in presence of bidder's representatives who choose to attend at Kolon Building Opposite DUWASA Head Office, PMU Office of the Ministry of Water (DODOMA HQ).

7. Late Bids, Portion of Bids, Electronic Bids, Bids not received, Bids not opened and not read out in public at the bid opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**The Addresses:**
**Physical address:**
**The Secretary, Ministerial Tender Board,**
**Ministry of Water**
**Kolon Building Opposite DUWASA Head office, PMU Offices**
**P. O. Box 456 Dodoma,**
**40473 Dodoma Email: pmu@maji.go.tz,**
**TANZANIA**

216333802

**Permanent Secretary,**
**Ministry of Water**

# Wabunge watoa somo upungufu wa mafuta

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE wameishauri serikali kuweka mikakati yenye tija ya kuondoa upungufu wa mafuta ikiwamo kuuza mbegu bora kwa bei nafuu.

Ushauri huo ulitolewa juzi kwenye kikao cha Kamati ya Kilimo, Uvuvi na Maji na wadau wa uzalishaji wa mafuta ya alizeti katika mradi wao wa Policy Analysis Group (PAG).

Mbunge wa Kuteuliwa, Dk. Bashiru Ally, alisema katika tatizo la alizeti kuna shida ya kupanga na kushauri mikakati ya kuondoa upungufu huo inatakiwa kwenda sambamba na mkakati wa kumaliza upungufu wa ngano na sukari.

Mbunge wa Muleba Kaskazini (CCM), Charles Mwijage, alisema mikakati ya kumaliza uhaba wa mafuta huenda isisaidie kitu kwa sababu imekuwa ya kutamkwa mdomoni.

Mwijage alisema wakati akiwa Waziri wa Viwanda aliweka mkakati wa kumaliza tatizo la mafuta ya kupikia nchini lakini hadi sasa mpango wake haujafanikiwa badala yake anaona wadau wanakuja na mpango mwingine bila kueleza wa kwanza walishindwa wapi.

"Lazima serikali iingize kwenye mipango yake ikiwemo kurudisha utaratibu hata wa kununua matrekta na kuwapa maeneo halisi ya kulima ili mtu mwenye shamba dogo awe na ekari walau 10," alisema.

Awali, Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Kilimo Timoth Mbaga, alisema soko la mafuta ni kubwa nchini kwani utoshelevu wa mafuta kwa sasa ni asilimia 45.

Alisema kiasi kinachobaki kinaagizwa nje na kwamba mikakati mizuri waliyonayo inaweza kufikisha malengo na ziada ikauzwa nje.

"Asilimia 95 ya wazalishaji na wakulima wa alizeti ni wakulima wadogo ambao wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa mbegu bora na hamasa ya kilimo cha zao la alizeti," alisema.



Ofisa Masoko wa Benki ya TPB, Dorothea Joseph (katikati), akitoa msaada wa mahitaji maalum kwa ajili ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Sinza Kitengo cha Mahitaji Muhimu, kwa Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Catherine Msese (kulia), Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Yatima wawekewa mazingira wezeshi

**Na Francis Godwin,** IRINGA

WATOTO yatima 51 wilayani Mufindi, Mkoa wa Iringa ambao baadhi yao wazazi wao waliofariki dunia kwa ugonjwa wa Ukimwi, wameanzishiwa makazi maalum kwa ajili ya kusaidia mahitaji ya msingi.

Wamejengewa makazi hayo katika Kijiji cha Igoda Kata ya Luhunga, huku ikielezwa kuwa mahitaji hayo ya msingi watakayopatiwa ni pamoja na elimu ya msingi hadi chuo kikuu.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM), Meneja wa mradi huo, Zilipa Mgeni, alisema kituo hicho kilianzishwa mwaka 2007, kikiwa na lengo la kusaidia watoto wanaotoka katika familia duni na yatima.

Alisema watoto hao wameendelea kupata malezi bora ikiwamo elimu na kupitia mradi wa YAM vijana na watoto wanaotoka katika familia duni zaidi ya 770 wanatarajia kusaidiwa na mradi huo kupata elimu ikiwamo ya ufundi wa uselemara kwa watoto wa kike pamoja na kuwapatia vifaa vya kuanzishia viwanda.

Mradi huo uko chini ya mradi wa Foxes Community And Wildlife Conservation Trust (FCWCT) unaofadhiliwa na Taasisi ya Deaconess Foundation ya Filind, na kwa wilaya ya Mufindi mradi huo unatekelezwa chini ya Halmashauri ya Wilaya.

Hata hivyo alisema mradi huo utatekelezwa kwa miaka minne kuanzia mwaka huu, na kwamba umeshaandaa wajumbe 160 kutoka vijiji 16 vya kata tatu za Ihanu, Luhunga na Mdabulo.

Alisema kuwa malengo ya mradi huo ni kuwahusisha vijana wenye ulemavu katika mfumo rasmi waajira na ujasiriamali, kuwezesha vijana walioopo katika mazingira magumu kujitegemea na kujisimamia wenyewe katika kutumia fursa zilizopo kwenye maeneo yao.

# Biteko awahakikishia wawekezaji wa madini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amewahakikishia wawekezaji na wadau wengine wa sekta ya madini mazingira bora ya uwekezaji na kufanya biashara.

Amesema hicho ni kitu muhimu kwa ustawi wa sekta hiyo na maendelo ya taifa kwa ujumla.

Waziri Biteko pia ameipongeza Benki ya NMB kwa kuwakutanisha wadau wa sekta ya madini na kuwapa fursa ya mafunzo ya biashara na kubadilishana mawazo kwa ajili ya ufanisi wao binafsi na kisekta kwa ujumla.

Biteko aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa "NMB Mining Club" ambalo ni jukwaa la kwanza nchini mahsusi la kuwahudumia wadau wa madini, akisema uwezeshaji wao unawezekana.

"Kama mnavyojua, lengo la Serikali ya Awamu ya Sita ni kuhakikisha tunaboresha mazingira ya wafanyabiashara ili kuwawezesha kukuza uchumi wa nchi yetu kupitia kodi, kutoa ajira na kuongeza mitaji.

"Tunaendelea na kusisitiza zoezi la kuongeza thamani ya madini lifanyike nchini ili taifa liweze kunufaika na utajiri wake mkubwa wa rasilimali hii na tayari Rais Samia Suluhu Hassan amefanya mambo mengi katika siku zake 100 za kwanza kwa ajili ya kuhakikisha hilo linafanikwa.

"Tumeshatoa leseni za usafirishaji madini ya dhahabu nne ambapo tayari kiwanda kimoja kimezinduliwa Mwanza na mambo mengine mazuri yanakuja," alisema Waziri Biteko.

Pia alisema "NMB Mining Club" ni ubunifu wa hali ya juu na kazi kubwa za aina hiyo ndizo zinaifanya benki hiyo kuwa kinara wa huduma na maarifa mapya sokoni. Kwa kuonyesha njia mpya ya kuwahudumia wachimbaji, NMB imetengeneza chanzo kipya cha mapato na kuwapata wateja wapya, alifafanua.

Alizichagiza benki nyingine kuiga mfano wa NMB na kuanza kuwakopesha kikamilifu wadau wa sekta ya madini na kuzitaka taasisi hizo kuunganisha nguvu kwa ajili ya kujenga uwezo wa kufadhili miradi mikubwa ya madini.

Klabu hiyo mpya inayojumuisha zaidi ya wadau wa madini 200 wa Kanda ya Kati imelenga kutoa mafunzo kuhusu maarifa ya biashara (elimu juu ya mipangilio ya biashara na elimu ya mwendelezo wa kitaalamu wa madini) na fursa ya kukutana na kubadilishana uzoefu wa kibiashara.

Wadau hao ni pamoja na wamiliki wa migodi, maduka makubwa ya vifaa vya uchimbaji, viongozi kutoka kampuni za madini, Kampuni ya Taifa ya Madini (Stamico), vyama vya wachimbaji wa kada zote na madalali.

Awali, Ofisa Mkuu wa Mikopo wa NMB, Daniel Mbotto, alisema mafunzo hayo yamekuja wakati biashara nyingi zikipata changamoto akitolea mfano wa kushuka kwa thamani ya bei ya Tanzanite kwenye soko la dunia.

# Madaraja, makalavati yote kujengwa

BUNGE limeelezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2022/23, mpango wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ni kujenga madaraja na makalavati yote.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Ummy Mwalimu, alisema hayo bungeni jana alipokuwa akitoa majibu ya nyongeza ya swali la Mbunge wa Nsimbo (CCM), Anna Lupembe.

Katika swali lake, mbunge huyo alitaka kujua mkakati wa serikali wa kukabiliana na tatizo la madaraja na makalavati ambayo yamekuwa wakisombwa na maji.

Aidha, alisema barabara ya Ilembo-Itenka ni muhimu kiuchumi na serikali imekuwa ikitenga fedha nusu nusu na mvua ikinyesha wananchi wa Itenka wanakuwa kisiwani.

"Lini sasa serikali itaweka fedha za kutosha ili barabara hii ikamilike kwa kuwa ni ya kiuchumi? Lini pia serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa madaraja matano badala ya makalavati?" Alihoji.

Akitoa majibu ya maswali hayo, Waziri Ummy alisema tayari wameshatoa maelekezo kwa Walaka wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) katika kila halmashauri kufanya usanifu wa madaraja na makalavati ili kujua gharama halisi.

"Tumeona Mheshimiwa Naibu Spika unaweza kutoa fedha tukajenga barabara, lakini kama madaraja na makalavati hayajajengwa hayapitiki maana yake tumefanya kazi bure. Kwa hiyo kipaumbele chetu mwakani tunataka tuelekeze kwenye madaraja na makalavati," alisema.

Wazuri Ummy aliwatoa hofu wabunge kuwa suala hilo limewekewa kipaumbele.

Katika swali la msingi, Lupembe alitaka kujua ni lini serikali itafanya ukarabati wa barabara ya kutoka Ilembo hadi Itenka ambayo ni muhimu katika uchumi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ofisi ya Rais-TAMISEMI, David Silinde, alisema barabara ya Ilembo-Itenka ina urefu wa kilomita 19.5 na katika mwaka wa fedha 2018/19, serikali iliifanyia matengenezo kipande chenye urefu wa kilomita 14 kwa gharama ya Sh. milioni 69.81.

Silinde alisema katika mwaka wa fedha 2019/20, serikali iliifanyia matengenezo barabara hiyo kipande chenye urefu wa kilomita 12 na ujenzi wa kalvati moja kwa gharama ya Sh. milioni 123.94.

Pia alisema katika mwaka wa fedha 2020/21, barabara hiyo imetengewa Sh. milioni 67.61 na hadi Mei 2021 ukarabati wa kipande chenye urefu wa kilomita tno na ujenzi wa makalavati matatu ulikuwa umekamilika na ukarabati wa kilomita tano unaendelea.

Alisema katika mwaka wa fedha 2021/22 serikali imetenga Sh. milioni 114.48 kwa ajili ya matengenezo ya barabara ya Ilembo-Itenka kipande chenye urefu wa kilomita nane na ujenzi wa makalavati mawili.



Naibu Spika, Dk.Tulia Ackson (katikati), akizungumza na watoto na walimu wa Kanisa la Moravian, Jimbo la Mashariki, Ushirika wa Uhuru, walipokutana nje ya viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mwekezaji mpya Mang'ula atafutwa

WIZARA ya Viwanda na Biashara na Ofisi ya Msajili wa Hazina, zimeandaa utaratibu wa kutafuta wawekezaji wapya watakaoviendesha viwanda vya Man'gula Machine and Mechanical Tools Limited.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Exaud Kigahe, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kilombero (CCM), Abubakar Asenga.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali ina mkakati gani wa kuanza uzalishaji katika kiwanda cha chuma Mang'ula.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini, pamoja na mambo mengine unalenga kufufua na kuendeleza viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo havifanyi kazi.

Alisema Mang'ula Mechanical Workshop (MMW) ni karakana iliyoanzishwa kwa msaada wa serikali ya China mwaka 1969.

"Karakana hiyo ilianzishwa kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa vipuri mbalimbali vya mitambo vilivyokuwa vinatumika wakati wa ujenzi wa reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA). Pamoja na utengenezaji wa vipuri, sehemu ya eneo la karakana hiyo ilitumika kujenga kiwanda cha Pre-Fabricated Concrete Manufacturing (PCM) kwa ajili ya kutengeneza mataruma ya zege na nguzo za zege," alisema.

Aidha, alisema karakana ya Mang'ula Mechanical & Machine Tools Co. Ltd (MMMT) ilirejeshwa serikalini mwaka 2019 kutokana na mwekezaji wake kushindwa kuendeleza kiwanda hicho kwa mujibu wa mkataba wa mauziano.

# Ahoji taasisi kutotumia ZIC

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Najma Murtaza Giga, amesema kumekuwa na kawaida kwa baadhi ya taasisi za serikali kutotumia huduma za Shirika la Bima la Zanzibar kwa kisingizio kuwa si la umma.

Akiuliza swali bungeni jana, Mbunge huyo alihoji serikali inalitambua shirika hilo kama la serikali au shirika binafsi.

Alihoji pia kama ni shirika la serikali, nini wito wa serikali kwa watendaji ambao wamekuwa wakikataa kutumia huduma hiyo kwa kisingizio cha kuwa si shirika la serikali.

Akijibu swali hilo kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Muungano na Mazingira, Hamad Hassan Chande, alisema shirika hilo limesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Bima Namba 10 ya Mwaka 2009.

Hamad alisema shirika hilo lina leseni hai yenye usajili Na. 00000704 inayoruhusu kufanya biashara ya bima za kawaida.

"Shirika hilo linamilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kwa asilimia 100, hivyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua kuwa shirika hilo ni mali ya SMZ na si shirika binafsi," alisema.

Alibainisha kuwa kwa kuwa Shirika la Bima la Zanzibar ni mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

"Wito wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa watendaji ambao wamekuwa wakikataa kutumia huduma zake kuendelea kulitumia shirika hilo kwa ajili ya kupata huduma za bima kama ambavyo wanalitumia Shirika la Bima la Taifa (NIC), hasa ikizingatiwa kuwa biashara ya bima nchini ni biashara huru na huria inayosimamiwa na Sheria ya Bima Na. 10 ya mwaka 2009 pamoja na kanuni zake,"



## RAIS SAMIA ALIVYONG'ARISHA DIPLOMASIA, UJIRANI MWEMA

Ukurasa 12





Ukurasa 14

**Rais Samia na bajeti inayowajali wanawake**

siasa
JUMATANO JUNI 30, 2021
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

# SIKU 100 IKULU...
## 'DAKTARI' SAMIA ALIVYOUTIBU UTAPIAMLO WA SIASA, UCHUMI

**Na Deogratias Mutungi**

SIKU 100 za Rais Samia Suluhu Hassan, zimekamilika zikiwa zimesheheni siasa zenye falsafa ya haiba, utu, demokrasia na uwajibikaji kisheria kwa misingi ya katiba.

Ilipofika Juni 26 tangu kuapishwa kwake Machi 19, kufuatia kifo cha mtangulizi wake John Magufuli (JPM), ndani ya utumishi wa umma Watanzania wameona mengi yenye mkondo chanya.

Rais Samia analivusha taifa kutoka lilipokuwa awali kuelekea kwenye siasa za utu, usawa, demokrasia na uwajibikaji.

Ni wazi kuwa zama za awamu ya tano ziligubikwa na "utapiamlo wa kisiasa" hivyo afya yake ilikwenda mrama na ni daktari wa kuliponya taifa kiafya, ametoa tiba kikamilifu kwa siku 100 za uongozi wake.

Ukiangalia kabla na baada ya kifo cha JPM unatagundua kuwa Rais katika utendaji wake, analenga zaidi kuitumia katiba ya Tanzania na si vinginevyo.

Amekuwa ni muwazi, mweledi sambamba na kurudisha imani kwa Watanzania kuhusu mifumo ya kisiasa na utawala bora iliyokuwa ikilalamikiwa hasa na upinzani.



Rais Samia Suluhu Hassan, akila kiapo cha urais Machi mwaka huu. Leo ametimiza siku 104 za kuliongoza taifa . **PICHA: MTANDAO.**

### KUBINYA UHURU

Serikali ya Magufuli ilifanya mambo makubwa kadri ilivyoweza, lakini ombwe lililojitokeza wakati wa utawala huo ni kubana misuli ya upumuaji wa "uhuru wa maoni" na ukosefu wa haki ya kujieleza.

Kubana haki hiyo kulizalisha mifumo mingine kama ukosefu wa demokrasia, uminywaji wa haki, viongozi wa umma kujichukulia sheria mkononi, kuumiza raia na ufisadi uliibuka kama alivyoripoti Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Wahusika walifanya hivyo wakiamini kuwa hakuna wa kupaza sauti kuwakosoa, aidha aliyejaribu kuwanyooshea kidole, hakusikilizwa na pengine alikiona cha moto.

Yote haya yalijitokeza kwa sababu mifumo iliyokuwapo katika utawala ilikuwa inajikita ndani ya mtizamo wa kufanya juhudi zote kuleta maendeleo, lakini kubinya uhuru wa maoni.

Jambo ambalo wasaidizi wa JPM walishindwa kulitambua na kushauri mamlaka ni kuwa hatima ya uongozi huo ungeleta jamii usugu na yenye upinzani imara, hivyo kuwa na ukosefu mkubwa wa fikra za kutaka maendeleo.

Badala yake raia walikuwa wakidai haki, uhuru wao na kulalamikia masuala mbalimbali dhidi ya dola.

Kisiasa na kiutawala hadi sasa hakuna nadharia inayoonyesha kuwa utawala usiojali demokrasia ulifanikiwa kujenga misingi imara ya maendeleo ya watu na vitu.

Zaidi inadaiwa unaimarisha chuki, hofu na machafuko ya ndani baina ya makabila, watu na hata vikundi na hivyo kuhatarisha amani ya watu na mali zao.

Muhtasari wa tafakuri hii unaonyesha wasaidizi wa JPM walipuuza na kudharau mantiki ya nguvu ya umma na kusimama katika nguvu ya dola. Kisiasa kuna utofauti mkubwa kinzani kati ya nguvu ya umma na ya dola, mara zote umma ni imara kuliko dola.

### AWAMU YA SITA

Kwa kuangazia ufanisi wa Rais Samia siku 100 kinachobainika ni ukweli kwamba Watanzania wengi walikuwa wakilia kwa miaka mitano iliyopita ni kunyimwa haki ya uhuru wa maoni na kujieleza.

Kimantiki hili ni eneo ambalo Rais Samia amechagua kuanza nalo na amefanikiwa kukonga nyoyo za Watanzania bila kujali itikadi za vyama vyao na kurejesha tumaini jipya la utawala wenye kuzingatia sheria, utu na nidhamu katika utumishi wa umma.

Bila shaka hili kwa Rais Samia halifanyiki kwa bahati mbaya bali anatambua misimamo na falsafa za mtangulizi wake zilisimamia nini, wapi na lipi, na kwa lengo gani?

Inawezekana maswali haya yasieleweke kwa sababu Rais Samia alikuwa Makamu wa Rais, lakini hoja na jibu ya swali hili iwe ni kuwa mabadiliko ya sasa ndani ya serikali ya awamu ya sita ni matokeo ya kile ambacho, kifalsafa hakukikubali.

Ndiyo maana Watanzania wapo hapo walipo kwa mabadiliko hayo yanayoendelea kufanywa na kama anavyosema kazi iendelee.

### USIKIVU, KUSHAURIKA

Aidha, ndani ya siku 100 za uongozi wa Rais Samia amedhihirisha kuwa ni kiongozi anayeshaurika na anayepokea ushauri si kutoka kwa watendaji na wasaidizi wake wa karibu ndani ya mifumo ya serikali bali pia kutoka hata nje.

Mara kwa mara katika mikutano yake na wadau kama wateuliwa, vijana, wanawake, wazee na viongozi wa dini amesikika akisema anapokea ushauri na atakwenda kuufanyia kazi.

Kwa dhana hiyo Rais ni msikivu na kiongozi anayeonyesha nia ya kusikiliza, kutatua na kutenda kadri alivyoguswa na kero iliyowasilishwa mbele yake. Kisiasa hii ni mojawapo ya sifa kuu ya uongozi, kwa yeye sio malaika kutokubali kushauriwa, hivyo kupata ushauri na kusikiliza raia anaowaongoza wanataka nini ni utimamu na tafsiri ya uongozi uliotokana na watu na ndiyo mantiki ya uwajibikaji wa kiongozi yeyote wa umma.

### DEMOKRASIA KIVITENDO

Kinachooneka bayana ni kwamba Rais ni mwanademokrasia wa kweli anayetawala ulingo wa siasa kwa vitendo na si kwa porojo za kisiasa.

Katika siku 100 kuna utashi wa kisiasa unaolenga kurudisha "amani ya kisiasa" kati ya chama tawala CCM na vyama vya upinzani.

Awamu ya tano ilionyesha udhaifu katika kusimamia mifumo, ilikosa uvumilivu wa kisiasa na fursa sawa baina ya upinzani kwani ulifika wakati waliishi kama mashetani na watu wasio stahili kupata haki kikatiba kama ilivyo kwa raia wengine.

Kuna wakati mwingine iliyeonekana kuwa mpinzani Tanzania ni sawa na 'mhaini' na kipo kipindi walilazimika kuhama vyama na kuingia upande mwingine.

INAENDELEA UK. 12





Waziri wa Mambo ya Nje, Liberata Mulamula. **PICHA: MTANDAO.**

# RAIS SAMIA ALIVYONG'ARISHA DIPLOMASIA, UJIRANI MWEMA

**Na Romana Mallya**

HIVI ndivyo Rais Samia Suluhu Hassan, alivyoweza kutumia siku 100 kuimarisha diplomasia kimataifa tangu kuapishwa Machi 19, mwaka huu kuwa Rais wa awamu ya sita.

Samia amevunja rekodi Afrika Mashariki na Kati kuwa mwanamama wa kwanza kushika wadhifa huo baada ya Rais wa awamu ya tano, Dk. John Magufuli, kufariki dunia Machi 17, mwaka huu kwa maradhi ya moyo.

Ukizungumzia diplomasia kimataifa huwezi kuiacha Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambayo kazi zake ni kuwakilisha nchi kimataifa, kuwasiliana na serikali za nje na taasisi za kimataifa mfano Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika na taasisi zake.

Aidha, ni kuendesha balozi katika nchi nyingine na kutoa visa kwa wageni wanaotaka kuja Tanzania kwa kushirikiana na wizara nyingine ndani ya nchi.

Ndani ya siku 100, Rais Samia amewateua wana diplomasia nguli kuiongoza wizara hiyo na miongoni mwao ni Waziri Balozi Liberata Mulamula, ambaye ni mbobezi katika masuala ya diplomasia kwa miaka zaidi ya 30 na amewahi kuhudumu kama balozi katika mataifa mbalimbali.

Amekuwa Katibu Mtendaji wa kwanza wa kongamano la kimataifa lililohusisha nchi 11 za Kanda ya Maziwa Makuu ya Afrika la Amani, Utulivu na Maendeleo (ICGLR) na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje.

Naibu Waziri ni Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, ambaye kuanzia Mei 2013 hadi Novemba 2019 alikuwa Balozi nchini Abu Dhabi, UAE, Pakistan, Iran na Bahrain.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Balozi Joseph Sokoine amekuwa Balozi Ubelgiji ambako pia aliwakilisha Umoja wa Ulaya, Luxembourg, Caribbean na nchi za Pacific.

Kwa safu hii ndani ya Wizara ya Mambo ya Nje ni udhihirisho kuwa Rais Samia amelenga kuimarisha diplomasia ambayo ndiyo sera ya mambo ya nje.

**NJE YA MIPAKA**

Mbali ya kuiimarisha wizara hii, Rais Samia ametumia siku 100 kwa kujenga diplomasia na pia ametembelea nchi jirani za Kenya, Uganda na Msumbiji.

Ametembelea Kenya na kufanya mazungumzo na Rais Uhuru Kenyatta na baadaye kulihutubia Bunge la Kenya linalojumuisha Bunge la Taifa na Seneti akiwa

> Aidha, wiki iliyopita Rais Samia, alikuwa jijini Maputo Msumbiji kushiriki mkutano wa dharura wa wakuu wa nchi na serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

ni Rais wa pili kulihutubia bunge hilo akitanguliwa na Rais mstaafu Jakaya Kikwete.

Katika hotuba yake, Rais Samia alitangaza sababu za ziara hiyo kuwa ni kukazia maeneo ambayo yalilegalega katika uhusiano wa nchi hizo.

Anaahidi kuendeleza miradi ya ushirikiano ikiwamo ujenzi wa barabara, ujenzi wa bomba la gesi la Dar es Salaam hadi Mombasa, ujenzi wa njia ya umeme ya kilovoti 400 kutoka Singida Tanzania kwenda Kenya, kukamilisha vituo vya huduma za pamoja mpakani.

"Kuongoza ni kuonyesha njia siyo kufunga njia. Kila mara panapotokea kutoelewana kati yetu tunadhoofisha uhusiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, bila kukusudia pia tunaathiri utangamano wa Afrika Mashariki, hivyo hatuna budi kuendelea kuelewana," sehemu ya hotuba yake ilisema.

Aprili mwaka huu, alizuru Uganda na kusaini mikataba mitatu yenye nia ya kuendeleza sekta ya mafuta na gesi ya Uganda, wakati wa ziara ya hiyo alikutana na mwenyeji wake Rais Yoweri Museveni.

Aidha, Mei mwaka huu, Rais Museveni alikuja Tanzania na kukutana na mwenyeji wake ikiwa ni mwendelezo wa kukamilisha makubaliano ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi, unaogharimu dola bilioni 3.5.

Mwezi huu Rais Samia amekutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Botswana, Dk. Mokgweetsi Masisi, jijini Dar es Salaam.

Aidha, wiki iliyopita Rais Samia, alikuwa jijini Maputo Msumbiji kushiriki mkutano wa dharura wa wakuu wa nchi na serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Mkutano huo ulijadili mengi ikiwamo kudumisha mtangamano, fursa mbalimbali za kiuchumi na matatizo ya kiusalama nchini Msumbiji.

**UTEUZI WA MABALOZI**

Rais Samia amefanya uteuzi wa mabalozi 23 watakaoiwakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali duniani miongoni mwao wakiwamo wanajeshi, wanahabari na mlimbwende wa Tanzania mwaka 1999.

Miongoni mwa kazi za mabalozi katika nchi wanazokwenda kuwakilisha ni kunadi na kufungua milango ya kiuchumi ya nchi kupitia mikakati ya diplomasia ya uchumi.

**MSIMAMO WA CORONA**

Mwezi Aprili, Rais Samia anatoa msimamo wa Tanzania dhidi ya corona akisema Tanzania siyo kisiwa haiwezi kujitenga na janga hilo na hii inatokana na mwingiliano wa kila siku wa watu duniani.

Aliunda jopo la wataalamu kuishauri serikali kuhusu corona na kuwasilisha ripoti yake na mapendekezo yake kwa utekelezaji.

# ALIVYOTIBU UTAPIAMLO WA SIASA

**INATOKA UK. 11**

Dhuluma dhidi ya upinzani zilitendeka kwa uwazi na mchana kweupe, hata hivyo kwa kipindi hiki cha siku 100 za Mama Samia upepo wa kisiasa umebadilika wapinzani wamepumua na siasa zinafanyika bila hiyana wala ghiliba au ubaguzi wa aina yoyote.

Na sasa vyama vya upinzani vinafanya siasa zao bila bugudha wala kero za rungu la dola.

Jicho la Rais katika siasa za usawa, uhuru na haki limetamalaki, kusudio lake la kutaka kukutana na vyama vya siasa na kuzungumza na wadau hao ni kusaka mustakabali wa taifa kisiasa na kurejesha misingi ya amani.

Lengo ni kufanya siasa safi, kudumisha udugu na siha njema na mafanikio ya kimkakati ya kutenda kile katiba inachoelekeza.

**KODI SAFI SI UBABE**

Mbali na hayo, Rais Samia ameonyesha weledi wa kusimamia mifumo ya ukusanyaji wa kodi kwa kutumia njia rasmi na kupata mapato salama. Mbinu zinazoeleweka bila kutumia mabavu na dhuluma.

Itakumbukwa taasisi za kikodi zilikusanya kodi kwa nguvu na dhuluma isiyokuwa na tija kwa taifa, hali hiyo ilijenga hofu na hivyo baadhi ya wawekezaji kukimbilia nje kuwekeza na kulikosesha taifa kukosa mapato.

Ufanisi wake upo wazi na sasa wawekezaji wanaanza kurejea nchini kutokana na mifumo kubadilika kwa kiwango cha hali ya juu. Kwa ujumla, kisiasa sera za Rais ni zenye tija na ustawi wa kiuchumi na kidiplomasia kwa maana ya diplomasia ya kikanda na kimataifa imekuwa ya kusaka fursa za kuwasaidia Watanzania kujikomboa kiuchumi na kiteknolojia kwasababu dunia inatuhitaji nasi tunaihitaji pia.

Aidha, uwepo wa misimamo dhidi ya corona kutoka kwa serikali ya awamu ya tano uliwatenganisha Watanzania na dunia kuonekana Tanzania ya wakati huo ni ya watu wasioeleweka wala kutabirika kwenye kuamini sayansi na mitishamba.

Misimamo ya sasa ya awamu ya sita dhidi ya corona unaitambulisha upya katika anga za kimataifa na kurudisha hadhi ya Tanzania kuwa hili ni janga la dunia hakuna anayeweza kujitenga na kujisimamia mwenyewe.

Ni wazi kuwa Rais Samia amefanikiwa kubadili upepo wa siasa za Tanzania ambazo zilionekana kuwa zina chuki, ubabe hata kwa mbinu za kukabiliana na corona kwani zilikuwa zikifuata mawazo na falsafa za mtu badala ya taasisi.

Kwa mantiki hiyo hazina tija kwa maendeleo ya Mtanzania wa kawaida zaidi ya kutengeneza chuki na ombwe la amani ndani yataifa.

Watanzania wanauona mwanzo mzuri aliouonyesha ndani ya siku 100, lakini kuna haja ya kujihadhari na wanasiasa wasaka tonge wanaoweza kutumia fursa ya maslahi yao binafsi kumpotosha na kumchonganisha na umma wenye imani na serikali yake.



UCHAMBUZI

# RAIS SAMIA HANA UTANI NA MAAMBUKIZI YA CORONA



Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa katika ziara ya kushtukiza katika Hospitali ya Rufani Mkoa ya Mwananyamala. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

HIVI karibuni Rais Samia Suluhu Hassan, ametembelea Hospitali ya Mwananyamala jijini Dar es Salaam, lakini

Mganga Mkuu Mfawidhi wa hospitali hiyo alimsihi asiingie kwenye wodi ya wagonjwa waliokuwa na matatizo ya upumuaji.

"Kuwa muwazi. Wagonjwa hawa wana maambukizi ya corona" Rais alimuuliza Mganga Mkuu aliyejibu "Ndiyo wana maambukizi ya COVID-19", na baada ya kauli hiyo Rais anawaambia wapigapicha wake waliokuwa wametangulia ndani ya wodi watoke haraka.

Hii linaonyesha anavyoguswa na corona na asingependa maambukizi yaendelee kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa wengine.

Rais Samia ametimiza siku 100 za kwanza Ikulu kama kiongozi akizingatia masuala nyeti yanayoikabili nchi, ikiwa ni pamoja na kubadilisha mtazamo wa jinsi ya kushughulikia maambukizi ya corona.

Ni kipindi ambacho dunia imeshuhudia Rais Samia, kupitia hotuba zake mbalimbali, akitoa sauti mpya juu ya masuala muhimu, ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa vyombo vya habari, siasa za upinzani na kutao vibali vya kazi.

Suala ambalo lingeweza kuvutia duniani ni uamuzi wa Rais kuunda kamati ya wataalamu kushauri serikali kuhusu corona na hatua zinazofaa kuchukua ili kuwaweka watu salama, uamuzi ambao aliufanya ndani ya wiki tatu baada ya kuingia madarakani.

Wakati wa kutangaza uamuzi huo alisema Tanzania haiwezi tena kupuuza virusi ambavyo vilikuwa vinaendelea kuangamiza dunia na kwamba Watanzania hawawezi kuishi peke yao kwani ni sehemu ya idadi ya watu duniani.

"Kuhusu suala la corona, nadhani ni lazima niunde kamati ya wataalamu kuliangalia kwa weledi na kisha niishauri serikali.

Haipaswi kunyamazishwa au kukataliwa au kukubalika bila utafiti wa kitaalamu," anasema wakati anawaapisha makatibu wakuu na manaibu mwezi uliopita.

Anaongeza: "Hatuwezi kujitenga kana kwamba sisi ni kisiwa, lakini hatuwezi kukubali kila kitu kilicholetwa kwetu. Hatuwezi kuendelea kusoma tu kuhusu corona katika sehemu nyingine duniani lakini Tanzania haieleweki."

Mnamo Aprili 6, mwaka huu, Rais Samia alitangaza kuunda kamati hiyo kwa msisitizo mkubwa juu ya kupambana na janga hilo kupitia njia za kisayansi.

Aidha, Mei 17 kamati ilikamilisha kazi ya tathmini ya ugonjwa huo na kuwasilisha ripoti kwa Rais na ikiwa na mapendekezo 19.

Wataalamu katika ripoti iliyowasilishwa kwa Rais Samia, wanadokeza kuwa Tanzania imepitia mawimbi mawili makubwa ya janga hilo na bado ina hatari ya kukutana na la tatu.

> Anapokutana na wazee wa mkoa wa Dar es Salaam, akiwa na wasaidizi wake walivaa barakoa akitoa mfano hai wa jinsi ya kujikinga na corona na katika mikutano yake yote ukiwamo wa wanawake mkoani Dodoma, wa vijana Mwanza, Maaskofu Katoliki na pamoja ule wa wanahabari muda wote anavaa barakoa.

Kamati hiyo ilitaka serikali iripoti habari sahihi juu ya janga hilo kwa raia wake na kwa Shirika la Afya Duniani (WHO), aidha, kuwasilisha nyaraka zinazohitajika kuhusu chanjo, ili kuanza kupokea dozi zake.

Kamati hiyo pia ilimtaka Rais Samia kuimarisha juhudi za kuzuia corona, kufuata maazimio ya kimataifa, kuimarisha uwezo wa utambuzi, kukamilisha mwongozo wa matibabu wa COVID-19 kwa wafanyakazi wa afya, kutumia dawa za jadi ikiwa tu zimethibitishwa na sayansi na kuanzisha vituo vya kutengeneza chanjo nchini.

Kamati hiyo pia ilitaka serikali itengeneze njia ya matumizi ya chanjo hiyo ndani ya nchi, wajumbe wa kamati wakiona kuwa hatua hizo zitasaidia kupambana na ongezeko la maambukizo ya corona ambayo yanaathiri mataifa mengi.

Kulingana na kamati hiyo, mpango wowote wa chanjo nchini unapaswa kuwapa kipaumbele wafanyakazi wa huduma za afya, wafanyakazi wa mbele, wale walio katika tasnia ya utalii na ukarimu, wazee (zaidi ya miaka 50), vikundi vilivyo hatarini wakiwamo wasafiri, lakini inashauri suala la chanjo linapaswa kuwa ni la uhuru kwa watu kuamua.

Ilipofika Mei 15 mwaka huu, Rais akatangaza kwamba serikali itatoa maamuzi iwapo itatoa chanjo ya corona au la. Baada ya ripoti hiyo ya Kamati ya Wataalamu, mabadiliko makubwa yalitangazwa ikiwa ni pamoja idhini kwa balozi na taasisi za kimataifa nchini Tanzania kuagiza chanjo ya corona kwa wafanyakazi wao.

Rais Samia baada ya kupokea ripoti hiyo anasema: "Balozi na mashirika ya kimataifa yameruhusiwa kuleta chanjo kwa raia na wafanyakazi wao kufuata taratibu za nchi zao na mashirika na vile vile kuondoa usumbufu katika kazi zao kwa sababu ya kutopewa chanjo. Chanjo hizo, hata hivyo, zitatolewa chini ya usimamizi wa Wizara ya Afya."

Katika mapendekezo hayo, kamati imependekeza njia ambazo zitaiwezesha serikali kupata fedha kutoka kwa bajeti ya kitaifa na washirika anuwai wa maendeleo ikiwa ni pamoja na mashirika ya kimataifa na sekta binafsi kwa vifaa vya matibabu, mafunzo na chanjo.

Rais Samia anaipongeza kamati hiyo na kumwelekeza Waziri wa Afya, Dk. Dorothy Gwajima, kuandaa hati itakayowasilishwa kwa Baraza la Mawaziri kwa majadiliano na baadaye serikali kutoa uamuzi kuhusu mapendekezo ya kamati hiyo.

Kuonyesha umma kuwa ni muhimu kuchukua hatua za tahadhari dhidi ya janga hilo Rais Samia daima anasisitiza kuvaa barakoa katika mikusanyiko yote ya umma.

Anapokutana na wazee wa mkoa wa Dar es Salaam, akiwa na wasaidizi wake walivaa barakoa akitoa mfano hai wa jinsi ya kujikinga na corona na katika mikutano yake yote ukiwamo wa wanawake mkoani Dodoma, wa vijana Mwanza, Maaskofu Katoliki na pamoja ule wa wanahabari muda wote anavaa barakoa.

Ni wazi kuwa jamii ya kimataifa ilikuwa na hamu ya kujua mtazamo wa Tanzania kuhusu chanjo na pia watu walikuwa wakingoja kujua ikiwa Rais atazingatia kutengwa na amri za kutotoka nje kama njia za kudhibiti virusi.

Tayari dunia imemuunga mkono Rais Samia kuhusu juhudi zake za kupambana na corona na wadau mbalimbali wameahidi kuisaidia Tanzania.

Itakumbukwa kuwa Machi 15, 2020, Tanzania ilitangaza mgonjwa wa kwanza wa corona mwanamama wa miaka 46 aliyewasili nchini kutoka Ubelgiji kwa ndege ya Shirika la Rwanda.

Msafiri huyo aliondoka nchini Machi 3, 2020 na kwamba kati ya Machi 5 na 13 alitembelea nchi za Sweden na Denmark na kurudi tena Ubelgiji na kwamba alipita uwanja wa ndege wa KIA.

Waziri wa Afya wa wakati huo, Ummy Mwalimu alieleza kuwa msafiri huyo alipofika KIA alifanyiwa ukaguzi na maofisa wa afya na hakuonekana na tatizo, baadaye alijisikia vibaya akiwa hotelini na kwenda Hospitali ya Mount Meru Arusha ambapo sampuli ilichukuliwa na kupelekwa maabara ya taifa Dar es Salaam kwa ajili ya uchunguzi.

Vipimo vya maabara vilithibitisha kuwa alikuwa na maambukizi ya corona na baada ya muda alipona na kuruhusiwa kwenda nyumbani kuendelea na shughuli zake. Tangu wakati huo serikali ilianza kuchukua hatua ikiwamo kufunga taasisi za elimu ili kudhibiti kuenea maradhi hayo.



# Rais Samia na bajeti inayowajali wanawake

**Na Mwandishi Wetu**



Rais Samia Suluhu Hassan, akikutana na wanawake kabla ya mkutano na kinamama jijini Dodoma. **PICHA:MTANDAO**

RAIS Samia Suluhu Hassan, hivi karibuni wakati anazungumza na wanawake mkoani Dodoma, anasimulia 'stori' ya maisha ya familia yake.

Hadithi hiyo inawagusa wengi kwani ilioonyesha wazi namna kulivyo na pengo la ufahamu wa masuala ya teknolojia baina ya wanawake na wanaume.

Anachosema kinawahusu wajukuu zake anaoishi nao, Ibra mwanamume na Samia msichana, akisema

akitaka kufanya lolote kwenye simu yake ambalo halijua au kuna kitu kakosea kubonyeza humwambia Ibra na mara moja kijana huyo mdogo hukirekebisha.

Lakini, akimwambia Samia amsaidie kitu fulani kwenye simu, haraka haraka atamwambia hajui na kumwita Ibra.

Hiyo ndiyo hali halisi kwa sasa ambayo mtoto wa kiume bila jamii kujua inajikuta ikimtayarisha zaidi kuingia katika dunia ya kidijitali ya sayansi na teknolojia kuliko inavyofanya kwa msichana.

Rais Samia angependa mjukuu wake Samia asiachwe nyuma katika zama hizi za kielektroniki au za sayansi na teknolojia, bali fursa sawa zitolewe kwa wanawake ili nao wapate nafasi ya kujifunza mambo mbalimbali ya kumudu maisha yao.

Kilio cha hivi majuzi cha baadhi ya wabunge jijini Dodoma cha kutaka wasichana zaidi wadahiliwe katika vyuo vya ufundi stadi (VETA) chanzo chake kipo katika usawa wa kijinsia ambao Rais Samia anausimamia.

Bunge la mwaka huu limeongeza pesa kwenye miradi ya maji vijijini ili kumpunguzia mwanamke muda wa kwenda kuchota maji ili ajishughulishe zaidi na mambo ya maendeleo ya familia yake.

Rais Samia anakubali kuwa bajeti yenye mrengo wa kijinsia inaweza kuanzisha uhusiano mzuri wa kufanya kazi na watendaji wa serikali katika wizara ambazo zimelengwa ili kurahisisha zaidi maisha ya wasichana na wanawake kwa ujumla.

Serikali tayari imetambua bajeti hiyo ambayo kwa kiasi kikubwa inajumuisha usawa wa kijinsia miongozo ya mbalimbali ya utoaji huduma katika jamii.

Mwaka 2001, miongozo ya bajeti iliagiza zaidi mawasilisho yote ya bajeti ya wizara, idara na wakala kutayarishwa kwa kuzingatia usawa wa kijinsia.

Tayari hazina wameanza kuweka mipango ya kujumuisha bajeti yenye mrengo wa kijinsia ili kutoa huduma kwa wote katika jamii.

Tathmini iliyofanywa hivi karibuni inaonyesha kuwa wahusika wa sekta iliyochaguliwa serikalini wameanza kunufaika na zoezi la ujumuishaji wa usawa wa kijinsia na mafunzo ya uwezo katika maeneo mbalimbali.

Kwa Rais Samia, Wizara ya Maji imekuwa ikijitokeza hasa katika kutumia shughuli za usawa wa kijinsia na imefaulu zaidi katika kuweka bajeti zao kijinsia katika huduma za majisafi na salama.

Serikali chini ya Rais Samia imeamua kutumia fursa inayopatikana kupitia mafunzo ya maofisa wa bajeti kwa mahitaji mapya ya Mfumo wa Matumizi ya Muda wa Kati pamoja na mafunzo ya kijinsia.

Shirika linalojishughulisha na Usawa wa Jinsia Tanzania (TGNP) na washirika wake wamekuwa wakialikwa na serikali ya Mama Samia na wafadhili kushiriki katika Mapitio ya Matumizi ya Umma pamoja na michakato ya Mkakati wa Misaada kwa Tanzania.

Kama mshiriki katika michakato hii, TGNP imetetea mabadiliko katika michakato ya uchumi mkuu, uwazi na uwajibikaji na watendaji wa serikali na ujumuishaji wa mitazamo anuwai ya kijinsia katika uamuzi wa serikali.

Bunge tayari limepitisha bajeti ya serikali ya Shilingi trilioni 36 kwa mwaka 2021/22, ambayo kwa namna moja au nyingine ni ya mrengo wa kijinsia, inayojali masuala yanayohusiana na maendeleo ya wanawake na wasichana.

Wadau wa jinsia wanafurahia bajeti ya mwaka huu kwa vile ina nafasi ya kuleta kichocheo cha uchumi shirikishi na maendeleo ya watu na pia kutoa mwelekeo wa mipango ya maendeleo kwa kila sekta inayowajali wanawake na wasichana.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, anamuunga mkono Rais Samia, akisisitiza kuwa kuna haja ya kutenga fedha kwa huduma nyingine za kijamii zinazohusiana na maendeleo ambayo yatachochea utoaji wa huduma, kama vile bima ya afya bure kwa wajane, wazee na wanawake maskini.

Lilian, pamoja na wadau wa usawa wa kijinsia walioshiriki kwenye mjadala wa Bajeti ya Kitaifa ya 2021/22 hivi karibuni anasema kuna haja kwa serikali kuanza kutekeleza Azimio la Abuja, (ambalo Tanzania imeridhia), kutenga asilimia 15 ya bajeti kuu kwa sekta ya afya.

"Wakati serikali inapoanza kutenga fedha kwa miradi na wizara tofauti, tunatoa wito kwa serikali na wadau wengine kuongeza uwekezaji katika kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuzuia magonjwa ili kupunguza gharama kubwa za matibabu." Anasema.

Akizungumzia kuhusu sekta ya maji, Lilian anatoa wito kwa serikali kupanua na kuongeza mtandao wa huduma ya maji safi na salama, kwa kuweka mikakati ambayo itakusanya fedha za kuendesha sekta hiyo.

"Wizara ya Maji inawajibika kutoa maagizo kwa idara za maji za mkoa ili kuwezesha upatikanaji wa maji kwa wajane, wazee kwa vipato vya chini zaidi, au hata bila malipo" anasema Lilian.

Halmashauri za wilaya zinapaswa pia kutenga ruzuku itakayokidhi mahitaji ya hedhi salama kwa wasichana katika shule za msingi na sekondari, anaongeza Mkurugenzi wa TGNP.

"Sasa ni wakati wa serikali kuanza kuboresha mazingira ya kujifunzia wasichana kwa kuondoa ushuru kwenye pedi, ili wasichana wa shule za msingi na sekondari waweze kuzipata," anasema.

Wabunge walijadili bajeti ya kitaifa kwa karibu wiki mbili, na wadau wa usawa wa kijinsia wameridhika kuwa vyuo vya ufundi na mafunzo vinaweza kusajili wasichana zaidi, kuwawezesha kupata ajira baada ya mafunzo.

Kwenye sekta ya kilimo, wadau wa usawa wa kijinsia wanapendekeza kutenga rasilimali za kutosha kulenga wanawake na vijana ili kuwapatia mikopo yenye masharti au ya riba ndogo na kuwapo na teknolojia zinazofaa za uzalishaji na pia kuwawezesha kufikia masoko kwa urahisi.

Katika bajeti ya mwaka huu, serikali imeahidi kuongeza juhudi zinazolenga kuunda vyanzo vya mapato, ambazo hazitaumiza au kuongeza mzigo kwa raia wa kawaida, hasa wanawake.

Wanawake nchini ni zaidi ya asilimia 51 ya idadi ya watu na ndiyo wanaotoa huduma za maji katika jamii kuanzia ngazi ya kaya pia wana jukumu la kufanya kazi karibu zote za kaya ikiwa ni pamoja na kutunza wagonjwa na watoto ambao mahitaji yao ya maji ni makubwa.

Chini ya uongozi wa Rais Samia, watetezi wa haki za wanawake na watoto wanatarajia nchini itapiga hatua kimaendeleo ikitoa huduma bora za kijamii kwa wanawake, wasichana na watoto.

> "Wakati serikali inapoanza kutenga fedha kwa miradi na wizara tofauti, tunatoa wito kwa serikali na wadau wengine kuongeza uwekezaji katika kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuzuia magonjwa ili kupunguza gharama kubwa za matibabu." Anasema.



## HABARI DODOMA

# Shirika laahidi elimu dawa za kulevya

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHIRIKA la Henry Jackson Medical Research International (HJFMRI) linalojihusisha na mapambano dhidi ya dawa za kulevya, limeahidi kuendelea kushirikiana na serikali katika kuelimisha jamii kuhusu tatizo la dawa za kulevya nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo, Sally Chalamila, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Dawa za Kulevya.

Chalamila alisema kuwa ushirikiano huo kati yao na serikali ni kuokoa maisha ya vijana, ambapo kwa vijana wa Nyanda za Juu Kusini wamefanikiwa kuwafikia waraibu 376 jijini Mbeya.

Alisema pamoja na kuwasaidia waraibu hao shirika limekuwa likifanya kazi ya kudhamini kliniki zinazotoa matibabu kwa ajili yao.

"Tutaendelea kufanya kazi kwa kushirikiana na mamlaka ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya pamoja na Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, shirika limekuwa likijihusisha pia kutoa tiba ya Methadone kwa waraibu wa dawa za kulevya na kuwafundisha namna ya kujilinda na maambukizi ya virusi vya Ukimwi," alisema.

Chalamila alisema HJFMRI imejipanga kutoa elimu mbalimbali za kupambana na virusi vya Ukimwi katika vituo vya afya 375 kwenye mikoa mitano.

Alitaja mikoa hiyo ni pamoja na Mbeya, Rukwa, Songwe, Katavi na Ruvuma na pamoja na kutekeleza miradi ya VVU na Ukimwi katika vituo 21 vya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ.)

Naye Mkuu wa Kituo cha Methadone mkoani Mbeya, Elius Bukuku, alisema kuwa mpaka sasa jumla ya waraibu 376 wanapata dawa kila siku.

Bukuku alisema kuwa mpaka sasa shirika limeweza kuwafikia waraibu 376 katika mkoa wa Mbeya na waraibu 40 Tunduma na wamezindua kliniki ya MAT katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya.



Naibu Meya wa Jiji la Dodoma, Emmanuel Chibago, akizungumza na vijana wa Kanisa la Angalikana Dinary ya Chamwino (hawapo pichani) kwenye bonanza la uchangiaji wa damu salama lililoambatana na uimbaji wa nyimbo za injili, jijini humo juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Tulia apigia debe siku ya mwanamke mwenye ulemavu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amewataka wabunge kuunga mkono hoja ya Tanzania kuwa na maadhimisho ya siku ya mwanamke mwenye ulemavu itakapopelekwa bungeni.

Aidha, amesema uwapo wa siku hiyo utasaidia kuwa na wigo mpana wa kujadili kero nyingi zinazowakabili wanawake wenye ulemavu tofauti na makundi mengine.

Dk. Tulia aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye kikao baina ya wabunge na wadau mbalimbali wa masuala ya ulemavu kilichoandaliwa na Taasisi ya Ikupa Trust Fund.

Alisema uwapo wa siku ya mwanamke mwenye ulemavu itatoa nafasi kama taifa kujadili kwa upana kero zinazowakabili.

"Siku hii ni muhimu sana kwani mwanamke mwenye ulemavu anakabiliwa na changamoto nyingi sana tofauti na makaundi mengine," alisema.

Aliwataka wabunge kuhakikisha kuwa hoja hiyo itakavyoletwa bungeni iungwe kwa asilimia 100, ili bunge liliridhe.

"Ili hoja yako ipite ni lazima waheshimiwa wabunge waiinge mkono hivyo basi natumaini wabunge mmetuelewa sisi wanawake wenye ulemavu na hoja hii ikija bungeni mtaiunga mkono kwa asilimia 100," alisema Dk. Tulia.

Naye Mwenyekiti wa Ikupa Trust Fund, Amon Mpanju, alisema kuwa uwepo wa siku hiyo utatoa fursa kwa wanawake wenye ulemavu kujadilia kwa kina kero zinazowakabili.

Alisema kama Bunge litaridhia uwapo wa siku hiyo basi Tanzania itakuwa nchi ya kwanza kuwa na maadhimisho ya siku maalumu ya mwanamke mwenye ulemavu.

"Hii hoja siyo yetu pekee yetu hata wenzetu wa shirika la kimataifa la Un-Woman pamoja na Shirika la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) wameunga makono sisi kuwa na siku hii rasmi," alisema Mpanju.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Twaweza, Aldan Eyakuze, alisema takwimu zinaonyesha kuwa mwanamke mwenye ulemavu anakabiliwa na kero mara mbili zaidi ya yule asiye na ulemavu.

Pia alisema wanawake wenye ulemavu wapo katika hatari ya kukumbana na ukatili kwa asilimia kubwa tofauti na wale wengine.

"Mwanamke mwenye ulemavu yupo hatarini kukumbana na changamoto ya ukatili mara tano ukilinganisha na wale wasio na ulemavu," alisema. Kwa upande wake, Mbunge wa Viti Maalum, Stella Ikupa, alisema ipo haja kwa jamii kupata elimu ili kubadili mitazamo juu ya watu wenye ulemavu.

"Tukipata siku hii itasaidia kujadili changamoto zetu hivi sasa sisi tunakabiliwa pia na changamoto ya kupendwa na kuwa na familia huku kuolewa imekuwa ni kazi hasa sisi wanawake," alisema Ikupa.

## W/biashara Dodoma, Singida wakutanishwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAFANYABIASHARA wakubwa na wadogo wa mikoa ya Dodoma na Singida wamekutanishwa katika Usiku wa Mtandao Thabiti kwa Ukuaji Endelevu wa Biashara.

Walikutanishwa na Benki ya NMB kupitia 'Business Executive Network' (BEN) na 'Business Club, huku jumuisho hilo likihudhuriwa na wafanyabiashara zaidi ya 700 kutoka Mkoa wa Singida na Babati (Manyara) kwa nyakati tofauti.

Katika usiku wa pamoja walitoa mafunzo ya uendeshaji wa biashara na mikopo, huku wakitangaza kiwango kikubwa cha mteja mmoja kuruhusiwa kukopa hadi Sh. 250 bilioni kutegemea na uwezo wake.

Meneja Mwandamizi wa benki hiyo kitengo cha biashara, Christopher Mgani, alisema kutokana na kukua kwa mtaji ndani ya benki, sasa wanaweza kutoa kiasi kikubwa na kwa marejesho ya muda mrefu kwa wateja wao.

Taarifa zinaeleza kuwa benki hiyo imefikia mtaji wa zaidi ya Sh. 7 trilioni huku ikiwa imeongoza kwa miaka nane mfululizo kuwa benki bora nchini.

Mgani alisema wameendelea kuboresha mikopo na mazingira ya ukopeshaji ambayo yamekuwa rafiki mkubwa kwa wafanyabiashara wa aina zote nchini huku wakisogeza karibu huduma za fedha kupitia NMB mkononi na Wakala zaidi ya 9,000 nchi nzima.

Kingine alifafanua kuhusu mikopo ya kujenga, kumalizia au kununua nyumb, akisema ni rafiki kwa kila mtu kulingana na kiwango cha mtaji wake na marejesho yake yanakwenda hadi miaka 15.

Mkuu wa kitengo cha biashara makao makuu, Alex Mgeni, alisema maboresho makubwa yamefanyika ndani ya benki na yote yakilenga kutoa unafuu kwa wateja wao kwa kuwa benki yake ndiyo kimbilio la wote.

Mgeni alisema wamefungua milango ya majadiliano na wateja wao siku 30 kabla ya kufanya marejesho pindi wanapohisi wamekwama na benki inafanya ufuatiliaji ili kuwasaidia kujikwamua.

"Kipaumbele chetu ni kuona wateja hawapati misukosuko katika biashara zao hasa kwenye marejesho kwani kukwama kwao ni kukwama kwa benki na sisi watumishi jambo ambalo hatukubali," alisema Mgeni.

Mmoja wa wateja, Neema Mandala, alisema katika maisha yake ya biashara anajivunia kuwa na benki hiyo kutokana na kupatiwa miongozo na maelezo ya watumishi.



# Mabadiliko hali ya hewa yashusha uzalishaji kahawa

**Na Nebart Msokwa,** MBOZI

WAKULIMA wa kahawa katika baadhi ya Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, wamesema kiwango cha uzalishaji wa zao hilo kimeshuka ikilinganishwa na wa awali kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Aidha, mabadiliko hayo yamesababisha ongezeko la magonjwa na kuongeza gharama za uzalishaji.

Waliyasema hayo juzi wakati walipokuwa wanapatiwa elimu maalumu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi inayotolewa na Shirika lisilokuwa la kiserikali la Hanns R. Neumann Stiftug Africans (HRNS), lenye makao makuu yake jijini Arusha.

Mmoja wa wakulima hao, Fraiton Mwazembe, alisema miaka ya nyuma walikuwa wanalima bila kutumia mbolea wala kupulizia dawa kwenye mashamba yao kutokana na ardhi kuwa na rutuba, lakini kwa sasa hali ni tofauti.

Alisema wakati huo walikuwa wanavuna mpaka tani mbili ya kahawa kwenye ekari moja, lakini kwa sasa wanashindwa kufikisha tani moja kutokana na hali ya hewa kubadilika na rutuba kupungua kwenye udongo.

Alisema kwa sasa magonjwa yanayoshambulia kahawa yapo mengi na baadhi yake huwa yanahitaji kupuliziwa dawa mara kwa mara ili kukabiliana nayo.

"Tunawaomba tu hawa wataalamu wetu wanaotoa elimu pamoja na serikali, watusaidie tupate dawa nzuri za kukabiliana na magonjwa haya maana mengine huwa hatuyaelewi kabisa," alisema Mwazembe.

Naye Amon Mwenga mkulima kutoka katika Kijiji cha Hezya, wilayani humo alisema kwa sasa mvua huwa inachelewa kuanza kunyesha hali inayosababisha maua ya kahawa kukauka kabla matunda hayajaanza.

Alisema wakati mwingine hata matunda yakianza huwa yanaanguka kabla hayajakomaa na kusababisha hasara kwa wakulima na wakiwauliza wataalamu wanaweleza kwamba tatizo hilo linaitwa CPD.

Aliiomba serikali iwasaidie mbinu za kitaalamu za kukabiliana na matatizo hayo ili kilimo cha kahawa kirejee kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Alisema baadhi ya wakulima wamekata tamaa ya kuendelea kulima kahawa na wameanza kulima mazao mengine yakiwamo ya chakula na ya mbegu za mafuta.

Ofisa Kilimo wa Kijiji cha Hezya, Geldath Paul, alisema kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaathiri kilimo cha kahawa, wameamua kuwaelimisha wananchi kuhusu mbinu bora za kilimo za kukabiliana na mabadiliko hayo.

Alisema kwa sasa joto linapanda kuliko ilivyokuwa miaka ya nyuma hali ambayo inaifanya ardhi ya wakulima ipoteze maji kwa haraka zaidi na kusababisha mazao kunyauka.

"Sasa sisi tunawaelimisha kutunza mazingira, waepuke kukata miti ovyo, tunawashauri pia hawa wakulima wenye mazao ya kudumu kama kahawa na migomba kuweka matandazo kwenye maeneo ya wazi," alisema Paul.

Kwa upande wake Ofisa Kilimo wa Shirika la HRNS, Godfrey Willgoad, alisema ili kukabiliana na matatizo hayo ya mabadiliko ya tabianchi ikiwamo kuhamasisha kilimo hifadhi.

Pia wakulima wanaelekezwa kutumia mbinu za kuweka matandazo shambani ili kupunguza upotevu wa maji kwenye ardhi hasa joto linapoongezeka.

Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe ni miongoni mwa ambazo uchumi wa watu wake unategemea zaidi kilimo cha kahawa na wakulima wanahitaji elimu ya kutosha ili waendelee kuzalisha kwa tija.



Mkulima wa kahawa katika Kijiji cha Hezya Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, akikoboa kahawa yake baada ya kuvuna juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Miundombinu ya elimu kuboreshwa kwa wanafunzi wote

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya, imesema itaendelea kuboresha miundombinu ya elimu kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi wote wakiwamo na wenye ulemavu kusoma bila vikwazo ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kuboresha sekta ya elimu.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Majuto Njanga, aliyasema hayo wakati alipokuwa akizungumza na wadau wa elimu kuhusu uboreshaji wa mazingira ya kutolea elimu maalumu na elimu jumuishi.

Alisema katika mkoa huo kuna vituo 19 vinavyotoa elimu maalumu kwa wanafunzi wenye ulemavu wa aina mbalimbali na mpaka mwezi Septemba, mwaka jana vituo hivyo vilikuwa na jumla ya wanafunzi 1,031.

Alisema serikali imekuwa ikivisaidia vituo hivyo kwa kutoa vifaa mbalimbali vya kufundishia wanafunzi wa makundi hayo pamoja na vifaa vya michezo kwa ajili ya kundi hilo.

Alisema Julai 9, 2020, serikali ya mkoa huo ilipokea vifaa mbalimbali vya kufundishia kujifunzia na vya michezo vikiwamo mashine za kuwasaidia kusikia wanafunzi wenye matatizo ya kusikia na mashine za kukuza maandishi kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu.

"Pia zilipokelewa mashine za kuchapia maandishi ya nukta nundu (Braille Papers), midoli ya aina mbalimbali na vifaa vingine vya kuchezea ili kuinua uwezo wa akili kwa watoto wenye mtindio wa ubongo," alisema Njanga.

Kadhalika, wameendelea kuhamasisha shule mbalimbali kuwa na miundombinu ya kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu kutopata shida ikiwamo kuweka maeneo maalumu ya kupita kwa wenye baiskeli za kusukumwa na viti vya kusukumwa.

Alisema viongozi wa ngazi zote wanatakiwa kusimamia na kuhakikisha miundombinu ya vyoo kwenye shule ili viwapo maalumu kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu.

# Benki ya damu yataja sababu uchangiaji kuwa finyu

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

TAARIFA za upotoshaji ambazo zimekuwa zikitolewa na baadhi ya watu kuhusu uchangiaji damu, zimetajwa kuwa miongoni sababu ya Benki ya Damu Salama kukabiliwa na uhaba wa damu kutokana na kusababisha watu wengi kutojitokeza kuchangia.

Hayo yalisemwa wakati wafanyakazi wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini nchini (TARURA), Mkoa wa Mbeya, walipojitolea kuchangia damu kwa hiari baada ya kikao kazi kilicholenga watumishi hao kupatiwa mafunzo ya kukabiliana na virusi vya Ukimwi (VVU), Ukimwi na magonjwa yasiyoambukiza, wilayani Kyela.

Baadhi ya wadau hao walizitaja kauli hizo kuwa ni pamoja na zizodai kuchangia damu kuna athari kiafya ikiwamo kupatwa na kizunguzungu na mwili kuzalisha damu kwa wingi kupita kiasi.

Mtaalamu wa huduma za maabara wa Kitengo cha Damu Salama, Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Anna Lwesya, alisema hakuna athari zozote kwa mtu mwenye sifa za kuchangia damu na kwamba sio kila mtu anastahili kuchangia damu.

Alisema watu wanaostahili kuchangia damu ni wenye umri wa kati ya miaka 18 na 65 na uzito kuanzia kilogramu 50 na kuendelea, wenye wingi wa damu kuanzia gramu 50 na mapigo ya moyo ya kawaida.

Alizitaja faida za uchangiaji damu kuwa ni pamoja na mchangiaji kuijua afya yake kutokana na vipimo atakavyofanyiwa kabla ya kuchangia na kisha kushauriwa na wataalamu namna ya kuishi.

"Halmashauri ya Wilaya ya Kyela pekee, uhitaji wa damu ni mkubwa, kama mnavyojua kwamba duniani kote hakuna maduka ya damu na badala yake ili mtu aongezewe damu ni lazima ichukuliwe kwa binadamu mwingine," alisema Anna.

Alizisihi taasisi mbalimbali zinapofanya vikao vyake kuwaita wataalamu wa damu salama na kuwahamasisha washiriki kujitolea kuchangia kama walivyofanya TARURA jambo alilosema litasaidia upatikanaji damu kwa urahisi na kuokoa maisha ya wahitaji.

Mmoja wa wawezeshaji kwenye mafunzo hayo, Dk. Sekiete Mndeme, kutoka Hospitali ya Wilaya ya Kyela, alikiri kuwapo kwa watu wanaopotosha umma kuhusu uchangiaji damu na kuwataka wanaobahatika kupata elimu sahihi kuwa mabalozi ndani ya jamii inayowazunguka.

Washiriki wa mafunzo hayo, Jackline Mwakatage na Mayungu Mbita, kutoka TARURA Halmashauri ya Jiji la Mbeya, walisema miongoni mwa mambo waliyonufaika kutoka kwa wawezeshaji ni pamoja na kupata uelewa wa kutosha namna sahihi ya uchangiaji damu na umuhimu wake.

Watumishi hao walisema ipo haja ya elimu sahihi ya uchangiaji damu kwa wananchi kuwa endelevu kupitia kampeni mbalimbali ili kuongeza uelewa kwa jamii na kuifanya aone ni jambo muhimu.





# ‘Tunashirikiana na washirika utoaji huduma bora za afya’

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Dk. Omar Dadi Shajak, amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo kuhakikisha wananchi wanapatiwa huduma bora za afya.

Akizungumza na Balozi wa Umoja wa Falme za Kiarabu nchini, Khalifa Almarzouqi, alipotembelea Hospitali ya Mnazimmoja, alisema nchi za Kiarabu ni miongoni mwa wadau wakubwa wa maendeleo hasa katika sekta ya afya Zanzibar.

Katibu huyo alieleza lengo la ziara ya balozi huyo ambaye ameambatana na maofisa kutoka Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii kutoka Abuu Dhabi ni kuona upatikanaji wa huduma za afya na kutafuta namna ya kuisaidia serikali ili kutoa huduma bora za afya kwa wananchi.

“Serikali pekee haiwezi kukamilisha huduma zote kwa wakati mmoja, hivyo wamekuja kutizama ili kuona namna ya kuisaidia serikali kadri ya uwezo wao katika maendeleo ya jamii na sekta ya afya,” alisema Katibu Mkuu.

Katika ziara hiyo pia wageni hao walipata fursa ya kutembelea eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya wilaya katika kijiji cha Mbuzini ambapo Katibu Mkuu alifafanua kuwa katika eneo hilo inatarajiwa kujengwa hospitali ili kupunguza msongamano katika Hospitali ya Mnazimmoja.

Aidha Katibu Mkuu alisema baada ya ziara hiyo maofisa hao wanatarajia kupeleka ripoti na kujadili namna bora ya kuisaidia Zanzibar katika sekta ya afya.

Wakati huo huo, Katibu Mkuu alimsimamisha kazi Ofisa Tabibu Msaidizi wa Kituo cha Wazee Welezo, Seif Hamad Suleiman kwa kosa la kulewa wakati wa kazi.



Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani Mnazi Mmoja, Dk. Msafiri Marijani (katikati), akiwa na Balozi wa Umoja wa Falme za Kiarabu nchini Tanzania, Khalifa Almarzouqi (kushoto), wakati maofisa kutoka Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii ya Abuu Dhabi, walipotembelea hospitali hiyo, mjini Zanzibar jana, kwa lengo ya kuisaidia SMZ katika sekta ya afya na maendeleo ya jamii. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Dawa za kulevya zateketezwa Z’bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMLA ya kilo 28 za dawa za kulevya aina mbalimbali zimeteketezwa katika kiwanda cha Sukari Mahonda Mkoa wa Kaskazini Unguja, chini ya ulinzi mkali.

Lengo la hatua hiyo ni kupambana na kutokomeza dawa za kulevya.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa ya Kulevya Zanzibar, Burhani Zubeir Nassor, alisema dawa zilizoteketezwa ni heroine, cocaine na bangi.

Alisema kutokomezwa kwa dawa hizo kumetokana na kumalizika kwa kesi 41 zilizokuwa zikiwakabili watu mbalimbali tangu mwaka 20016-20018.

Alisema zoezi la kuteketeza dawa za kulevya litaendelea kwa kadri dawa hizo zitakapokamatwa na baada ya kumalizika kwa kesi zake.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais, Dk. Sada Mkuya, alisema vita dhidi ya dawa za kulevya ni endelevu na watahakikisha watu wanaojishughulisha na biashara hiyo haramu wanatiwa mbaroni.

Alisema matarajio makubwa ni kuundwa kwa kikosi cha kupambana na dawa za kulevya, ambacho kitakuwa na nguvu kamili ya mamlaka na majukumu ya kusimamia tatizo hilo.

Mwenyekiti wa kamati ya kuteketeza dawa za kulevya, Muumini Khamis Kombo, alisema dawa zote yanazokamatwa baadaye huteketezwa.

**Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais, Dk. Sada Mkuya, alisema vita dhidi ya dawa za kulevya ni endelevu na watahakikisha watu wanaojishughulisha na biashara hiyo haramu wanatiwa mbaroni.**

# Zuhura Othman awafunda wajasiriamali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKE wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Zuhura Othman Masoud Othman, amewataka wahitimu wa mafunzo ya ujasiriamali kuyatumia ili kuleta mabadiliko na maendeleo ya taifa.

Alitoa ushauri huo katika mahafali ya kumaliza mafunzo ya ujasiriamali kwa wajasiriamali 17 waliohitimu mafunzo yao yanayofadhiliwa na Serikali ya Marekani.

Alisema ni jambo la msingi kwa wajasiriamali hao kuyafanyia kazi kivitendo mafunzo hayo na kutoa ushirikiano kwa kuwaelimisha wanawake wenzao, ambao hawakupata fursa hiyo ili waweze kunufaika na kuboresha biashara zao kwa lengo la kuinua kiuchumi na taifa kwa ujumla.

“Uwajibikaji unahitaji matumizi mazuri ya rasilimali fedha, taaluma, muda na watu na rasilimali nyingine,” alibainisha.

Aliwasisitiza wahitimu hao kuonyesha utaalamu, uweledi, juhudi za kufanya kazi kwa kufuata miongozo ya kitaalamu kama walivyoelekezwa kwani kinyume cha hayo wamepoteza rasilimali zilizotumika katika kuendesha mafunzo hayo.

Alisema serikali ya Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, imedhamiria kuwawezesha wajasiriamali hasa wanawake ili kuinua uchumi wao kupitia shughuli rasmi.

Aidha, alisema kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi imekuwa ikipokea ushauri kutoka kwa wajasiriamali na wawekezaji kwa lengo la kuboresha mazingira ya kibiashara Zanzibar.

Akizungumzia kero zinazowahusu wanawake, alisema serikali imejipanga kuwahudumia wananchi wote hasa wajasiriamali wanawake kwa kutatua changamoto zao kwa haraka ili kuendelea kuweka mazingira bora ya kutekeleza shughuli zao za kiuchumi.

Naye Mwakilishi wa Balozi wa Marekani nchini, Tanzania, Amy Hart Vrampas, alisema serikali yao imedhamiria kuwainua wajasiriamali wanawake, hivyo mafunzo hayo ni sehemu ya kuwasaidia wanawake kujitegemea.

Alisema, lengo lao ni kutafuta njia ya kuwawezesha wanawake wa Tanzania kujiajiri kupitia uzalishaji wa bidhaa mbalimbali.

Mkuu wa Programu ya AWE Zanzibar, Rashid Mwinyi, alibainisha kwamba taasisi yao ina lengo la kupunguza kudumaza kwa biashara za wajasiriamali hapa nchini na kusaidia uimarishaji wa biashara za wanawake na kukabiliana na soko la ajira.

Mratibu wa mradi wa AWE Tanzania, Dk. Victoria Kisyombe, aliiomba serikali kuwawezesha wahitimu hao kwa kuwapatia ruzuku kutoka mifumo ya serikali ili kuendeleza biashara zao.



Aliyekuwa Rais wa Afrika Kusini, Jacob Zuma alipokuwa mahakamani kabla ya hukumu yake. **PICHA: MTANDAO**

# Kifungo cha Zuma jela mjadala mzito

**Na Christina Mwakangale**

WANASHERIA, wanasiasa na wanaharakati nchini wameeleza hukumu ya aliyekuwa Rais wa Afrika Kusini, Jacob Zuma kuwa inatoa funzo kwa viongozi wa Afrika.

Kwamba wanatakiwa kuheshimu mihimili mingine ikiwamo Mahakama, licha ya nafasi na nyadhifa walizonazo kabla na baada ya kustaafu.

Zuma, alihukumiwa kifungo cha miezi 15 jana, mjini Johannesburg, Afrika Kusini, baada ya Mahakama Kuu kumkuta na hatia ya kukosa kuhudhuria vikao vya kamati iliyokuwa inachunguza tuhuma za rushwa dhidi yake.

**OLENGURUMWA**

Mratibu Kitaifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Wakili Onesmo Olengurumwa, akizungumza na Nipashe jana kuhusu suala hilo, alisema, viongozi mbalimbali barani Afrika wakiwamo marais wanatakiwa kuheshimu mihimili mingine kama Mahakama bila kujali madaraka waliyonayo.

Alisema utii wa mihimili ikiwamo mahakama inapotolewa wito wa kuitwa kwa ajili ya mahojiano ni muhimu viongozi hao kutii.

"Rais haitakiwi kudharau mihimili mingine kama mahakama, wito wa mahakama usipuuzwe. Mahakama Afrika Kusini imefanya kujifunza kwa wengine.

"Ulinzi wanaowekewa marais hata baada ya kustaafu haimaanishi kutotii mihimili. Ingawa mifumo ya nchi za Afrika bado haitekelezi jukumu kama hilo, ila tumepata funzo Afrika," alisema Olengurumwa.

**PROFESA KAMANGA**

Prof. Khoti Kamanga alisema umuhimu wa kuwa na Mahakama ya Katiba ambayo haisiti kulinda Katiba, kwamba pasi kujali anayekiuka msingi iliyomo kwenye Katiba, ikiwamo utawala wa kisheria na usawa mbele ya sheria.

"Kwa kifupi, hukumu hii inarudisha heshima ya Mahakama na kwa upande mwingine onyo kwa wanaotumia madaraka vibaya," alisema Prof. Kamanga.

**ZITTO KABWE**

Zitto Kabwe, Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, akizingumza na Nipashe jana, kuhusu hukumu hiyo, alisema Katiba ni chombo muhimu duniani.

"Ni kwamba ukuu wa Katiba ni muhimu kwenye nchi zote duniani. Afrika Kusini imeonyesha mfano wa ukuu wa Katiba," alisema Zitto.

**CEGODETA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, alisema ipo haja ya kupatikana kwa Katiba mpya, ili sheria ziheshimike barani Afrika.

"Kuwapo kifungu cha kushtakiwa iwapo rais aliyestaafu atafanya tofauti, mfano viongozi wa Afrika baadhi hukaa madarakani muda mrefu wakijua sheria haziwabani," alisema Ngawaiya.



Zitto Kabwe

Alisema Katiba zikibadilishwa zitawaonya viongozi waliopo madarakani kuheshimu sheria kabla na baada ya kustaafu.

**MASHTAKA**

Mahakama ya Juu ya Pietermaritzburg ilitoa hati ya kukamatwa kwa Zuma, baada ya kushindwa kufika mahakamani kukabiliana na mashtaka kuhusu rushwa dhidi yake.

Ilielezwa kuwa hati hiyo ingefanya kazi ikiwa Zuma angeshindwa kuhudhuria kesi yake iliyotarajiwa kuanza Mei. Zuma alikabiliwa na makosa 16 ya kughushi, rushwa, ulaghai na utakatishaji fedha ukihusisha biashara ya silaha ya thamani ya mabilioni ya dola iliyofanywa tangu miaka ya 1990.

Rais huyo wa zamani alifanikiwa kukwepa shutuma za rushwa dhidi yake kwa zaidi ya miaka 10.

Hati ya kukamatwa kwake ilitolewa baada ya kushindwa kufika mahakamani kwa ajili ya kusikiliza kesi yake.

Jopo la wanasheria wake waliwasilisha nyaraka wakisema mteja wao alikuwa mgonjwa na alikuwa akipatiwa matibabu nje ya Afrika Kusini.

Jaji Dhaya Pillay alihoji maelezo yaliyo kwenye nyaraka za matibabu za Zuma zilizowasilishwa na mawakili wake mahakamani.

Zuma alikabiliwa na mashtaka kadha wa kadha ya rushwa ikihusisha malipo 783 yenye utata anayodaiwa kupokea kutoka kwa aliyekuwa mshauri wake wa masuala ya fedha, Schabir Shaik.

Madai hayo pia yalirejelea mkataba wa silaha uliofanyika miaka ya 1990 na kampuni moja ya masuala ya ulinzi ya nchini Ufaransa.

**HUKUMU JANA JOHANNESBURG**

Jaji Sisi Khampepe, ambaye alitoa hukumu hiyo jana, alisema hukumu hiyo si ya lazima iwapo Zuma, atazingatia maagizo ya mahakama na kuanza kuhudhuria vikao vya kamati inayomchunguza.

Mwenyekiti wa kamati ya mahakama inayomchunguza Zuma, Raymond Zondo, alikuwa aliiomba mahakama kumfunga Zuma miaka miwili jela kwa kususia vikao vya kamati yake.

Tangu mwaka 2018, Zuma amekuwa akikabiliwa na kesi ya rushwa ambayo, amekuwa akikanusha kwa madai ya kuchochewa kisiasa.

Alikuwa akifika mahakamani akikabiliwa na shutuma za ufisadi ambazo amekuwa akizikanusha.

Wafanyabiashara walishutumiwa kwa kula njama na wanasiasa kushawishi mchakato wa kufanya maamuzi ya serikali ya Rais huyo wa zamani alijitokeza mara moja kwenye uchunguzi wa kile kilichojulikana kama kukamatwa kwa serikali, ingawa alikataa kujitokeza baadaye.

Katika suala tofauti la kisheria, Zuma alikataa hatia mwezi uliopita katika kesi yake ya ufisadi iliyohusisha makubaliano ya silaha ya Dola bilioni tano kutoka miaka ya 1990.

# Man United yakaribia kumnasa Camavinga

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imepanga kukutana na mawakala wa kiungo wa Rennes, Eduardo Camavinga wiki ijayo ili kujadili uhamisho wake wakati wa dirisha la uhamisho wa kipindi cha majira ya joto.

Klabu kadhaa zimetajwa kupendezwa na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa na ripoti ya hivi karibuni ilidai kwamba, Man United ilimfanya kuwa kipaumbele cha uhamisho kabla ya msimu wa 2021/22.

Kwa mujibu wa RMC Sport, 'Mashetani Wekundu' hao wameelezea nia yao kwa kijana huyo mwenye umri wa miaka 18 na wanapanga kukutana na wawakilishi wa kiungo huyo wiki ijayo.

Ripoti hiyo inadai kwamba, kipaumbele cha Camavinga ni kujiunga na Paris Saint-Germain, lakini maofisa wa Man United wanatarajia kumshawishi ahamie kwa mabingwa hao mara 20 wa Ligi Kuu England.

Mfaransa huyo amefunga mabao mawili na kutoa pasi za mwisho katika mechi 82 kwa timu yake ya sasa.






# NISTELROOY ATABIRI MAKUBWA KWA DEPAY

**AMSTERDAM,** Uholanzi

AKIWA sehemu ya makocha wa Frank de Boer katika kikosi cha Uholanzi kwenye Euro 2020, Ruud van Nistelrooy amesema anasubiri kwa hamu kuona makali ya Memphis Depay kwenye klabu yake mpya ya Barcelona.

Nisterlrooy amefanya kazi kwa karibu na straika huyo wa zamani wa Lyon na Manchester United, na sasa amesajiliwa na Barcelona.

Wakati alipokuwa akifanya kazi ndani ya Uholanzi tangu Desemba 2019, wakati Ronald Koeman alipomuita kwenye nafasi ya ukocha msaidizi, na sasa kwenye Euro 2020, amemshuhudia Depay karibu zaidi.

"Memphis ni mtu ambaye naona ana umakini maalum," alisema Nistelrooy akinukuliwa na vyombo vya habari.

"Ana hamu ya kuwa bora katika timu anayocheza. Ni jambo ambalo ninaona ni zuri kulitazama."

Uholanzi ilitolewa kwenye hatua ya 16 na Jamhuri ya Czech kwenye michuano ya Euro 2020.

"Memphis na Georginio Wijnaldum wameonyesha kwamba wanaweza kufanya lolote kwa klabu yoyote kubwa ni dhahiri na takwimu hazina uwongo," aliongeza Van Nistelrooy.

# *Messi aweka rekodi mpya Argentina*

**CUIABA,** Brazil

LIONEL Messi ameweka rekodi ya kuwa mchezaji aliyeichezea mechi nyingi zaidi timu ya Taifa ya Argentina.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, Messi alianza kwenye mchezo wa Copa America dhidi ya Bolivia pale kwenye dimba la Arena Pantanal, Jumatatu.

Na hiyo ilimfanya kufikisha mechi 148 alizoichezea Argentina na kuizima ile ya awali iliyowekwa na mlinzi Javier Mascherano aliyecheza mechi 147, ambaye kwa sasa amestaafu.

Messi alianza kuichezea Argentina mwaka 2005 kwenye mchezo wa kirafiki wa ushindi wa 2-1 dhidi ya Hungary.

Lakini Messi kwenye mchezo huo alitolewa nje kwa kadi nyekundu baada ya kumpiga kiwiko mpinzani wake.

Straika huyo wa Barcelona, pia anashikilia rekodi ya ufungaji bora wa muda wote kwa Argentina akifikisha mabao 73.

Kwa sasa anatafuta kuivunja rekodi ya Pele kwa wachezaji wa mataifa ya Amerika Kusini ambaye aliifungia Brazil mabao 77.

Pia anaweza kuivunja rekodi ya Sergio Livingstone wa Chile ya kucheza mechi nyingi zaidi (34) kwenye mashindano ya Copa America, huku yeye Messia akiwa amecheza mechi 31 hadi juzi.

Diego Maradona alifunga mabao 32 katika mechi 87 kwa Argentina, ikiwamo kwenye ushindi wa Kombe la Dunia mwaka 1986.

Messi, licha ya kuwa na takwimu nzuri, lakini hajawahi kushinda taji lolote kubwa na Argentina.

Alikuwa mshindi wa pili na Argentina kwenye Kombe la Dunia mwaka 2014 na mara mbili katika michuano ya Copa America mwaka 2015 na 2016.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE ALIA KUTESEKA USINGIZI KUKOSA PENALTI

### Huzuni kubwa kwa kutolewa, nitashindwa kulala, nilitaka kuisaidia timu lakini...

**BUCHAREST,** Romania

KYLIAN Mbappe ameomba radhi kwa kukosa penalti wakati Ufaransa ikitolewa kwenye Euro 2020 mbele ya Uswisi, huku nyota huyo akisisitiza atapata wakati mgumu sana kupata usingizi usiku.

**Penalti ya Mbappe iliokolewa na Yann Sommer, ambaye alikuwa shujaa wakati Uswisi wakipata mikwaju 5-4 dhidi ya Ufaransa ambao ni mabingwa wa Kombe la Dunia na wakatolewa kwenye hatua ya timu 16-bora, juzi.**

Ufaransa ilikuwa na nafasi nzuri wakati ikiongoza kwa mabao 3-1 dhidi ya Uswisi, lakini dakika 15 kabla ya mchezo kumalizika, wakajikuta mabao yote yamesawazisha na kuwafanya wacheze dakika za nyongeza 30 na baadaye penalti.

Ufaransa walianza kuwa nyuma kwa bao moja kabla ya Karim Benzema kusawazisha na kufunga la pili huku Paul Pogba akifunga la tatu.

Uswisi walishuhudia nyota wao, Ricardo Rodriguez akikosa penalti wakati wakiwa na nafasi ya kuongoza 2-0 mapema kipindi cha kwanza, kabla ya Haris Seferovic kufunga bao la pili na Mario Gavranovic la tatu na kufanya ubao kusomeka 3-3.

Mbappe alikuwa akipiga penalti ya mwisho, lakini golikipa Sommer akaiokoa na Ufaransa wakashindwa kutinga hatua ya robo fainali.

"Ni ngumu kufunga ukurasa," alisema Mbappe kupitia ukurasa wake wa Instagram - ambaye alikuwa na mashuti mengi zaidi (14) bila kufunga kuliko mchezaji yeyote kwenye mashindano ya Euro 2020.

"Huzuni kubwa ni baada ya kutolewa, hatukuweza kufikia malengo yetu.

"Nasikitika kwa penalti ile. Nilitaka kuisaidia timu, lakini nilishindwa.

"Nitakuwa na wakati mgumu wa kulala usingizi, lakini ukweli ni kwamba kuna hatari nyingi kwenye mchezo huu ninaoupenda sana.

"Najua kwamba, nyinyi mashabiki mmekatishwa tamaa na hili, lakini ningependa kuwashukuru kwa sapoti yenu na mara zote nimekuwa najiamini kupitia nyinyi.

"Kitu cha muhimu ni kwamba tutakuwa imara zaidi kwenye changamoto ya mechi zinazokuja. Hongera na kila la heri kwa Uswisi."

## ZISIKUPITE

### RAMOS AZISUBIRISHA CITY, PSG

MLINZI wa Hispania, Sergio Ramos, 35, anachunguza ofa alizopata kutoka kwa Manchester City, PSG na Bayern Munich kabla ya kufanya uamuzi kuhusu hatima yake. ***(ESPN)***

### BALE KURUDI REAL MADRID

KLABU ya Tottenham Hotspur haina mpango wa kuongeza mkataba wa mkopo kwa Gareth Bale, 31, kwa msimu wa pili na mchezaji huyo anatarajiwa kurudi katika klabu yake ya Real Madrid, ambako amebakiza mkataba wa miezi 12. ***(Evening Standard)***

### CAMAVINGA HANA OFA

RENNES imesema haijapata ombi lolote la kiungo wa kati raia wa Ufaransa, Eduardo Camavinga, 18, licha ya mchezaji huyo kuhusishwa na Manchester United na PSG. ***(Metro)***

### PATRICIO KUPEWA MKATABA

AS Roma inakaribia kukubali kumpa mkataba golikipa wa Ureno, Rui Patricio, 33, kutoka Wolves. ***(Sky Sports)***

### BELOTTI AWANIWA ARSENAL

ARSENAL inamnyatia mshambuliaji wa Torino, Andrea Belotti, 27, lakini AC Milan, Fiorentina, Napoli na Roma, zote zinamuwania. ***(Tuttosport, via 90Min)***

### SANTRIANO AGOMBEWA EPL

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan na Uruguay, Martin Satriano, 20, anazivutia klabu za Arsenal, Everton, Tottenham na Everton. ***(Mail)***

### BERARDI SASA LULU ULAYA

LEICESTER City ni miongoni mwa klabu kadhaa zinazomtaka mshambuliaji wa Italia, Domenico Berardi, 26, anayeichezea klabu ya Sassuolo ambaye kwa sasa yupo na kikosi cha Italia kwenye Euro 2020. ***(Gazzetta Dello Sport, via Leicester Mercury)***

### GILMOUR KUONDOKA CHELSEA

NORWICH City inakaribia kumsajili kwa mkopo kiungo wa kati wa Scotland, Billy Gilmour, 20, kutoka Chelsea. ***(Sky Sports)***

### OTAVIO ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL huenda ikamsajili mshambuliaji wa Porto na Brazil, Otavio mwenye, 26, kwa kiasi cha pauni milioni 34. ***(Star)***

### COX ATAKIWA ASTON VILLA

ASTON Villa na Norwich zote zinajaribu kumwania golikipa wa England, Matthew Cox, 18, kutoka Klabu ya AFC Wimbledon. ***(Football Insider)***

### ROBERTO NA MKATABA MPYA

BARCELONA inafikiria kumpa mkataba wa miaka miwili beki wa Hispania, Sergi Roberto, 29, ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2022. ***(Marca)***

# WASHINDI CRDB MARATHON 2021 KUONDOKA NA MIL. 45/-

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imetenga kiasi cha Sh. milioni 45.4 kwa washindi 32 wa msimu wa pili wa mbio za CRDB Marathon 2021.

**Tayari CRDB imesajiliwa na Chama cha Usajili na Upimaji wa Mbio za Kimataifa (AMIS), kwa kushirikiana na Shirikisho la Kimataifa la Mchezo wa Riadha (World Athletics).**

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Mawasiliano wa benki hiyo, Tully Mwambapa, alisema kwa mwaka huu zawadi zimeongezwa ili kuendana na hadhi ya kimataifa ambayo CRDB Bank Marathon imepewa.

Mwambapa alisema: "Mwaka huu siyo marathon tu, hata zawadi pia ni za kimataifa zaidi. Tumejipanga kutoa zawadi nono kwa washindi, kwa mbio kubwa za kilometa 42, mshindi wa kwanza atapata Sh. milioni tano, wa pili Sh. milioni tatu, mshindi wa tatu milioni mbili na wa nne milioni moja".

Huku akiwataka Watanzania kujitokeze kwa wingi kujisajili katika mbio hizo, Tully alisema wingi wa zawadi mwaka huu unatokana na kuongezeka kwa namba ya washiriki na kwamba matarajio ni kupata washiriki 5,000 kutoka ndani na nje ya nchi.

Akizungumzia fursa zitokanazo na mbio hizo ambazo sasa hivi zimesajiliwa kimataifa, Tully alisema zitakwenda kuchochea uchumi wa Jiji la Dar es Salaam na kulitangaza.

Tully alisema mbio hizo pia zinalenga kuwaleta pamoja Watanzania kuchangia watu wenye uhitaji katika jamii pamoja na kutatua changamoto nyingine zinazoikabili jamii.

Alisema mwaka huu lengo ni kukusanya Sh. milioni 500 ambazo zitaelekezwa katika kusaidia watoto wenye uhitaji wa upasuaji wa moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), ujenzi wa Kituo cha Mawasiliano katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, pamoja na kampeni ya utunzaji mazingira ya "Pendezesha Tanzania"

Mkurugenzi wa Uendeshaji wa EFM na TVE, Denis Busulwa (Ssebo), alisema kampuni yao inajivunia kuwa washirika wa CRDB Bank Marathon kutokana na mbio hizo kujikita zaidi katika kuhamasisha watu kusaidia jamii.

Katibu Mkuu wa Shirikikisho la Riadha Tanzania, Jackson Ndaweka, aliipongeza Benki ya CRDB kwa kuandaa mbio hizo kwa viwango vya kimataifa huku akimhakikishia Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB, Tully Mwambapa kuwa zawadi zote zitabaki nchini.

Kujisali na kuchangia katika CRDB Bank Marathon washiriki wanatakiwa kutembelea katika tovuti rasmi ya mbio hizo www.crdbbankmarathon.co.tz.




Mkurugenzi wa Mawasiliano Benki ya CRDB, Tully Mwambapa (wapili kushoto) akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kutangaza zawadi zitakazotolewa kwa washindi wa CRDB Bank Marathon 2021. Kutoka kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa Kampuni ya Udalali wa Bima ya Benki ya CRDB, Wilson Mnzava, Mkurugenzi wa Uendeshaji wa EFM, Denis Busulwa (Ssebo) na Msimamizi wa Mbio za Kimataifa kutoka Chama cha Usajili na Upimaji wa Mbio za Kimataifa (AMIS), Norrie Williamson. **NA MPIGAPICHA WETU**

# 'Pilato' wa Simba, Yanga hadharani leo

**Na Adam Fungamwango**

WAAMUZI watakaochezesha mechi ya watani wa jadi kati ya Simba na Yanga Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, wanatarajiwa kuwekwa hadharani leo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almasi Kasongo, amesema wanatarajia kupewa majina hayo kutoka kwa Kamati ya Waamuzi na wakiyapata tu, watayatangaza leo hii.

Kasongo alisema hayo baada ya kulizwa kama waamuzi watakaochezesha mechi hiyo ni wale wale waliokuwa wachezeshe mchezo huo Mei 8, mwaka huu ama wamebadilishwa.

Waamuzi waliokuwa wachezeshe mechi iliyopita ni Emmnuel Mwandembwa wa Arusha, ambaye alikuwa awe kati, Frank Komba wa Dar es Salaam, alipangwa kuwa mwamuzi msaidizi namba moja na wa pili ni Hamdani Said kutoka Mtwara, wakati mwamuzi wa akiba alipaswa kuwa Ramadhani Kayoko kutoka Dar.

"Siwezi kulizungumzia leo kama ni wale wale au wengine. Sijawasiliana na Kamati ya Waamuzi, ila wametuahidi hadi kufika kesho (leo) watatuambia. Walikuwa wanamalizia kikao chao, wakimaliza watatufahamisha na wakifanya hivyo, basi tutawafahamisha," alisema Ofisa Mtendaji huyo.

Mechi hiyo ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara ilikuwa ichezwe Mei 8 uwanjani hapa, lakini ilishindwa kupigwa kutokana na mkanganyiko wa muda wa kuanza.

Awali, mechi ilikuwa ichezwe saa 11:00 jioni, lakini baadaye ilipelekewa saa 1:00 usiku kitu ambacho viongozi wa Yanga walipinga, wakapeleka timu saa 11:00 jioni kama ilivyopangwa na kuondoka muda mfupi baadaye.

Timu ya Simba ilifika uwanjani kwa ajili ya kucheza saa 1:00 usiku, lakini hawakuwakuta wenzao. Na wakidhani kuwa wanaweza kupewa ushindi, ikatangazwa uwanjani hapo kuwa mechi hiyo imeahirishwa na itachezwa siku nyingine.

## Uhamiaji yapanda Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Uhamiaji imekata tiketi ya kupanda Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao wa 2021/22 baada ya kufikisha alama 47 kwenye msimamo wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja.

Uhamiaji imefikisha pointi hizo na kukata tiketi hiyo baada ya juzi katika mchezo wake wa mwisho wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya New King kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Kinyasini Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Mpinzani wa karibu wa Uhamiaji, timu ya Taifa Jang'ombe, katika mchezo wake wa mwisho juzi, iliambulia kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Gulioni FC, hivyo kubaki na alama zake 43. Hata kama Taifa Jang'ombe ingeshinda mechi hiyo na Uhamiaji kushinda bado isingeweza kupanda Ligi Kuu kwa kuwa ingezidiwa pointi moja.

Katika ligi hiyo ambayo ilishirikisha timu 12, mbili zimeshuka daraja ambazo ni Idumu FC na Mchangani United, ambapo kuelekea msimu mpya, sasa zitacheza ligi za mikoa yao.

## TAFF waanza kunoa waamuzi wa Afcon

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka kwa Watu Wenye Ulemavu Tanzania (TAFF), limefungua kozi ya ukufunzi wa waamuzi ikiwa ni maandalizi ya kuelekea mashindano ya Afrika (Afcon) yatakayoanza Novemba 26 hadi Desemba 4, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Kozi hiyo ambayo imeanza jana jijini Dar es Salaam na ikitarajiwa kumalizika Julai 2, mwaka huu, imeandaliwa na Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya na itahusisha waamuzi mbalimbali kutoka mikoa ya Tanga, Morogoro, Mwanza, Pwani na Dar es Salaam.

Michuano ya Afcon kwa watu wenye ulemavu itashirikisha mataifa 16 huku Tanzania wakiwa wenyeji wa michuano hiyo ambayo itatoa timu nane zitakazokata tiketi ya kwenda Kombe la Dunia.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Rais wa TAFF, Peter Sarungi, alisema kozi hiyo itatoa waamuzi ambao watasimamia na kuchezesha mashindano ya Afrika, kwa sababu Tanzania watakuwa wenyeji wa michuano hiyo.

# Michezo

Jumatano Juni 30, 2021

Nipashe



United yakaribia kumnasa Camavinga UKURASA 22

TUTA TUTANI...




Kipa wa Uswisi, Yann Sommer, akiicheza penalti ya mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe wakati wa changamoto ya 'matatu' baada ya timu hizo kutoka sare ya mabao 3-3 kwenye mechi ya hatua ya 16-bora ya michuano ya Euro 2020 iliyopigwa Uwanja wa National Arena jijini Bucharest, Romania juzi. Uswisi ilisonga mbele kwa penalti 5-4. **PICHA: MTANDAO**

# Karia aupiga mwingi uchaguzi wa urais TFF

## ●●● Abaki mgombea pekee, waliokatwa Hawa na Mgeusa wakiri kukosa sifa huku sasa wakiahidi...

**Na Saada Akida**

RAIS anayetetea nafasi yake kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wallace Karia, 'ameupiga mwingi' kwa kukidhi vigezo vyote vilivyokuwa vinatakiwa, hivyo kuwa mgombea pekee katika uchaguzi huo utakaofanyika jijini Tanga Agosti 7, mwaka huu, imeelezwa.

**Safari ya Karia kuruka vihunzi hivyo kwa kukidhi matakwa ya kanuni za uchaguzi huo zilianza wakati wakiwa wagombea sita waliochukua fomu na kurejesha, wakiwamo Ally Mayay Tembele, Oscar Oscar, Ally Saleh, Hawa Mniga na Evans Mgeusa.**

Hata hivyo, wagombea hao walichujwa na kubaki watatu, Hawa, Mgeusa na Karia, ambaye jana Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TFF, Benjamin Kalume, alimtangaza kuwa mgombea pekee kutokana na wagombea hao wawili kukosa sifa.

Akizungumza na Nipashe jijini Makao Makuu ya TFF jana, Kalume alisema kwa mujibu wa uchaguzi ibara ya tisa imewaondoa Hawa na Mgeusa kwa kukosa vigezo ikiwamo uzoefu katika kazi.

Alisema kamati yake ilifanya usaili na Hawa pamoja na Mgeusa wote walikiri kutokidhi vigezo vilivyowekwa ikiwamo kuongoza mpira wa miguu kwa miaka mitano.

"Kulingana na kanuni hizo, wagombea hao wawili wameenguliwa katika kuwania uchaguzi huo huku tukimpitisha Karia kutokana na kukidhi vigezo, hivyo kwa mujibu wa Katiba na Kanuni mpya ya TFF zilizobarikiwa katika mkutano mkuu, mgombea anayebaki pekee katika nafasi yoyote hatapigiwa kura bali atathibitishwa katika mkutano mkuu siku hiyo ya uchaguzi," alisema Kalume.

Hata hivyo, wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti jana, wagombea hao waliokatwa, walieleza kuridhishwa na uamuzi uliofanywa na kamati hiyo kutokana na kutokidhi kigezo hicho cha uzoefu.

"Nimeridhishwa na maamuzi ya kamati, sitasonga mbele wala kukata rufani kwa sababu sina vigezo ikiwamo cha kuongoza mpira kwa muda uliowekwa wa miaka mitano, sasa ni somo kwangu na kujipanga upya kwa ajili ya kwenda kugombea miaka ijayo," alisema Hawa.

Kwa upande wa Mgeusa alisema:"Mchakato umeenda vizuri. Tumeenda kwenye usaili vizuri, lakini suala la vigezo la kuongoza soka kwa muda huo ni kweli sijafikisha hivyo naacha uchaguzi usonge mbele siwezi kwenda kukata rufani."

Aidha, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi huo, Kalume, aliwataja wagombea wa nafasi ya wajumbe wa Kamati ya Utendaji wa TFF waliopitishwa kugombea kwa Kanda zote sita ni Athuman Kambi, Lameck Nyambaya, Hosseah Lugano, Khalifa Abdallah, Zakayo Mjema, Abousufian Sillia, James Mhagama na Mohammed Mashango.

Wengine ni Hamis Kitila, Mohammed Aden, Osuri Kosuri, Vedastus Lufano, Salum Alli, Blassy Kiondo, Issa Mrisho na Kenneth Pesambili.

## Messi aweka rekodi mpya Argentina

**CUIABA,** Brazil

LIONEL Messi ameweka rekodi ya kuwa mchezaji aliyeichezea mechi nyingi zaidi timu ya Taifa...




HABARI UK. 21

## 'Pilato' wa Simba, Yanga hadharani

**Na Adam Fungamwango**

WAAMUZI watakaochezesha mechi ya watani wa jadi kati ya Simba na Yanga Jumamosi...

HABARI UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >